# Nipashe

Jumamosi Juni 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580623

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





SIKU 100 IKULU

**Samia** apeleka kicheko sekta mama ya elimu

UKURASA 4



**Mbaroni** tuhuma kuua shangazi kwa mapanga

UKURASA 5

**Mbappe kutua Madrid baada ya Euro 2020**

UKURASA 22

# CORONA III IPO NCHINI




• **Rais** Samia aomba viongozi wa dini... *Endelea uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Kurasini mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Ndugai aonya stahiki za Lissu

UKURASA 3



## Mahakama Kuu ilivyotengua hukumu vigogo CHADEMA

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA SC YATANGULIA FAINALI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Maaskofu wataka utawala wa sheria

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kupokea majukumu hayo mapya, akimwomba kuimarisha utawala wa sheria nchini.

Katika mkutano wa baraza hilo na Rais Samia mkoani Dar es Salaam jana, kiongozi huyo wa kanisa alisema baraza hilo linamwahidi kumpa ushirikiano katika kuliongoza taifa.

Alisema kuwa katika kuimarisha utawala wa sheria, ni muhimu kujenga taasisi za utawala wa sheria.

Rais huyo wa TEC alisema mwaka 2016 sera mbalimbali zilibadilishwa katika uendeshaji wa vyuo vikuu ambazo zilisababisha hasara kwa taasisi ikiwamo maslahi ya watumishi kutolipwa kwa wakati kwa sababu idadi ya wanafunzi ilishuka.

Alisema watoa huduma katika sekta muhimu walivunjika moyo katika kutoa huduma ya elimu na kwenda kutafuta maslahi ya muhimu kwao.

Askofu Nyaisonga alisema wamepata hasara katika vyuo vilivyokuwa vimeanzishwa hasa vijijini ikiwamo mikoa ya Ruvuma, Kagera na Mtwara.

Katika sekta ya afya, alisema umeibuka ushindani badala ya kufanya kazi kwa ushirikiano, hali iliyodhoofisha huduma zinazotolewa na kanisa katika kutatua kero za afya nchini.

Askofu Nyaisonga alisema shule pia zinatakiwa kuwa na leseni ya biashara ilhali lengo siyo kuendesha shule kibiashara bali kutoa huduma bila kujali uwezo wa wazazi.

Alimwomba Rais Samia kufanya mapitio ya makubaliano yaliyopo katika taasisi zinazotoa huduma kwa ubia na serikali na kutambua taasisi hizo kama wadau wakubwa wa kutoa huduma bila kujinufaisha.

Pia, alisema baadhi ya maeneo ya ardhi ya taasisi za dini yaliyopo kwa ajili ya kilimo, yameanza kuchukuliwa na serikali kwa madai kuwa yana miradi ya serikali. Kuhusu kodi, Askofu Nyaisonga alisema hospitali za mashirika ya dini hazipati unafuu wa kulipa kodi ya mapato ya ajira.

Alisema kumekuwapo na kikwazo cha hospitali za mashirika zilizokubali kubeba majukumu yote ya watumishi, lakini hawalipwi chochote kutoka serikalini.

**ASKOFU KILAINI**

Askofu Msaidizi wa Jimbo la Bukoba, Dk. Method Kilaini, alieleza historia ya TEC na ushirikiano wao na serikali tangu zama za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alikumbusha kuwa mwaka 1969, Mwalimu Nyerere alizitaifisha shule zote na wakati huo TEC ilikuwa na shule za sekondari 1,420, shule za msingi 44, vyuo vya ualimu vinane, shule za ufundi vya wavulana 15 na wasichana 48.

Askofu Kilaini alisema kuwa baada ya utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi, waliruhusiwa tena kujenga shule na kanisa lilianza tena kuwekeza kwenye elimu kwa kujenga shule.

Kuhusu Sekta ya Afya, Askofu Kilaini alikumbusha kuwa mwaka 1968, walipoadhimisha miaka 100 ya Ukristo, TEC ilikuwa na hospitali 68, zahanati 75 na kanisa limekuwa likishughulikia kipekee afya ya wanawake ndiyo sababu walikuwa na vituo vya kujifungulia 74.

Alisema baraza linaendesha hospitali 60 nchini ikiwamo ya Rufani ya Bugando na zenye hadhi ya mikoa saba, zahanati 296 na vituo vya afya 108 na jumla ni 464 wakati asilimia 80 ya hospitali zote zipo vijijini. "Asante sana mama unapothamini hospitali za vijijini kwa sababu siyo vitega uchumi, bali vinatoa huduma wakati mwingine bure na siyo kukamua kodi," alisema.



Waombolezaji wakitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mkurugenzi Mwenza wa Gazeti la Jamhuri, marehemu Mkinga Mkinga, Viwanja vya Mnazi Mmoja mkoani Dar es Salaam jana na baadaye kusafirishwa kwenda Chato, mkoani Geita kwa mazishi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia: Corona ipo

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema wimbi la tatu la corona lipo nchini, akiwaomba viongozi wa dini wasaidie kuzungumza na Watanzania ili kuepuka vifo vingi.

Mkuu wa Nchi huyo alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) ambalo lilimwalika kwa mazungumzo.

Rais Samia alisema dunia inakabiliwa na janga hilo na kukumbusha kuwa tangu mwanzo kanisa hilo limekuwa na msimamo thabiti katika kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo.

"Niwaombe maaskofu na viongozi wengine wa dini, pamoja na masuala mengine mnayohubiri kwa waumini, msisahau kukumbusha waumini kuhusu umuhimu wa kujikinga na kuchukua tahadhari zote dhidi ya corona.

"Kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba, tusiache kutumia kila kitakachotukinga na maradhi haya ili kuepusha vifo vya makundi.

"Kama tunavyojua, duniani sasa hivi kuna wimbi la tatu la corona, tumetoka wimbi la kwanza Tanzania limekwenda, tukaingia wimbi la pili, tumekwenda nalo na sasa kuna wimbi la tatu," alisema.

Rais Samia alisema ishara ndani ya nchi zinaonekana na tayari kuna wagonjwa wameonekana katika wimbi hilo hilo la tatu.

"Kama mnakumbuka siku niliyotembelea Hospitali ya (Rufani ya) Mwananyamala, kuna wodi Daktari Mfawidhi alikuwa ananiingiza, akaniambia humu kuna wagonjwa wenye matatizo ya kupumua.

"Nikamwambia 'hebu kuwa muwazi ni Covid (Corona)?', akaniambia 'ndiyo Covid'.

"Wakati huo wapigapicha wangu walikuwa wameshatangulia, nikawaambia 'nyie tokeni haraka huko'.

"Niseme kwamba hili jambo bado lipo, tusijiachie, tuchukue tahadhari zote, tunaomba viongozi wa dini mliseme hili kwa sauti kubwa kwa waumini ili tujiepushe na vile vifo vya makundi," Rais alisisitiza.

Alisema ni muhimu viongozi wa dini kumwomba Mungu ili aendelee kuwaepusha na kuwapa hifadhi yake hasa kwa janga hilo la corona kwa kuwa ndiye muweza wa yote.

Huku akinukuu maandiko ya Biblia, Rais Samia alisisitiza rai yake hiyo kwa viongozi wa dini, akifafanua:

"Ndiyo maana ninahimiza tumwombe Mungu atuwekee mkono, atufunike na mbawa za malaika wake ili tuhifadhike na maradhi haya."

Rais Samia alisema pamoja na kinga zote na njia zote za kitaalamu watakazotumia, Watanzania wasisahau kurudi kwa Mungu kumwomba aepushe na janga hilo.

Pia aliahidi kuvifanyia kazi vikwazo vinavyolikabili kanisa katika kutimiza majukumu yake ikiwamo kutoa huduma afya na elimu.

Kuhusu ombi la vyuo vya kanisa kurejeshewa programu zilizokuwa zikifundisha, Rais Samia alisema walifikia uamuzi huo mwaka 2016 kupitia Sheria ya Vyuo Vikuu na kanuni zake, wakilenga kulinda ubora wa elimu baada ya baadhi yake kutokidhi viwango kwa kukosa wahadhiri wa kutosha na miundombinu.

Rais Samia alisema miongoni mwa walioshiriki katika kutunga kanuni hizo ni Padri Charles Kitima na kuieleza TEC kuwa kama ni mchawi wanaye huko ndani.

"Vyuo vile vitafunguliwa, kuna vingi vilifungwa lakini baada ya marekebisho vikafunguliwa, vyuo hivyo vitafunguliwa," aliahidi.

Katika hatua nyingine, Rais Samia alilipongeza Kanisa Katoliki kwa kuvigeuza vyuo vyake viwili vya Songea na Bukoba kuwa vyuo vya ufundi kwa sababu vinaendana na azma ya serikali kuimarisha elimu ya ufundi.

Alitoa wito kwa viongozi wa dini kuendelea kuwahimiza wananchi kudumisha amani na umoja wa kitaifa, kuchapa kazi kwa bidii pamoja na kutimiza wajibu wa kuwa waadilifu na waaminifu bila kusahau kulipa kodi.

Virusi vya corona vililipuka kwa mara ya kwanza mwishoni mwa mwaka juzi huko Wuhan, China na mgonjwa wa kwanza aliripotiwa nchini Machi 16, mwaka jana.

# Ndugai aonya upotoshaji madai stahiki za Lissu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA Job Ndugai amesema Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itaanza kuwaita na kuwahoji watu wanaolipaka Bunge matope.

Amesema watu hao wanajumuisha wanaosambaza taarifa alizoziita za upotoshaji kwamba kuna mtu fulani ana madai ya malipo yake bungeni.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa kauli hiyo bungeni jijini Dodoma jana, akisisitiza taasisi hiyo ni miongoni mwa vyombo ambavyo hazimwonei mtu na kama mtu ana madai yeyote, anapaswa kufuata utaratibu.

Kauli hiyo ya Spika Ndugai ni majibu yake kwa mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Mbagala (CCM), Abdalah Chaurembo, aliyelalamika kuchafuliwa na chombo kimoja cha habari kuhusu mgawanyo wa mali za lililokuwa Jiji la Dar es Salaam.

"Wale wa mitandao, tunaomba sana mlipe heshima Bunge, na kama mtu mmoja ana mambo yake, anapaswa kufuata taratibu zilizopo.

"Serikali haidaiwi chochote katika lile tangazo, ni la zamani na lilishafanyiwa kazi, halituhusu hivi sasa, hata wizara inajua hilo.

"Mtu anaamua kuchanganya umma, hafanyi chochote, halafu wengine wanajiita wachungaji. Huko mbele, tutaanza kuwaita baadhi maana Kamati ya Maadili ipo palepale.

"Tumevumilia vya kutosha, maana tunakaribia kuchoka. Hii hali ya kupakanapakana matope pasipokuwa na mbele wala nyuma, tunaomba waje taasisi ya Bunge ina namna ya kuji-defend (kujilinda), wawe makini na taarifa zinazohusu Bunge hasa za upotoshaji," alionya.

Spika Ndugai aliendelea: "Jana (juzi), kuna tangazo fulani lilitoka la majina mengi kwamba limetolewa na TRA (Mamlaka ya Mapato).

"Katika majina yale ya wizara mbalimbali, yapo na majina ya wabunge wa Bunge la 11 lililomaliza muda wake.

"Ninadhani mliliona kwenye mitandao, kumbe lengo lao ni kumfuatilia mtu mmoja tu wanayemtaka wao, kuonyesha ana madai fulani bungeni, lakini orodha imetolewa ndefu na wakaanza kumshambulia Spika (Ndugai) kule na kuchonganisha na kadhalika."

Alibainisha kuwa tangazo hilo linalosambaa katika mitandao ya kijamii ni la mwaka 2018.

Katika maelezo yake Spika Ndugai, alisema hakuna anayelidai Bunge, 'awe ni mbunge wa upinzani, wawe wachache au wengi, hakuna anayedai'.

Akionyesha kukerwa na tangazo hilo, Ndugai alisisitiza: "Na kama mtu ameishiwa huko Ulaya au wapi, si aseme tu kuliko kusingizia Bunge kila wakati kwamba kuna madai?

"Hata huyo mtu wao (hakumtaja jina), alilipwa kila kitu ila malipo yake yalipokwenda benki, benki ilichukua zote.

"Unajua watu wengine wanataka kila wakati mje na vitu kumuumbua mtu. Kwa nini mnaamini amini mtu vitu ambavyo havipo?"

Juzi, kulisambaa taarifa kwenye mitandao ya kijamii zikionyesha serikali imelipa madai ya muda mrefu ya watumishi wakiwamo wabunge wa Bunge la 11 lililofikia tamati Juni mwaka jana.

Miongoni mwa waliotajwa katika tangazo hilo linalolalamikiwa na Spika Ndugai, ni la Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Lissu, mbunge wa zamani wa Sindiga Mashariki, kwa sasa anaishi Ubelgiji barani Ulaya.



Katibu Mkuu mpya wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Kenani Kihongosi, akizungumza na vijana wa umoja huo, alipokuwa akijitambulisha kwenye viwanja wa makao makuu ya CCM, Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mahakama yatengua hukumu vigogo CHADEMA

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetengua hukumu ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kuwaachia huru vigogo wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wakiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe na Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk. Vicent Mashinji.

Kadhalika, Mahakama Kuu imeamuru Sh. milioni 350 walizolipa faini Mbowe na wenzake, zirejeshwe. Hukumu hiyo ilisomwa jana na mahakama hiyo na Jaji Ilvin Mgeta, aliyekuwa akisikiliza rufani hiyo.

Akichambua hukumu hiyo, Jaji alisema ameangalia hukumu ya Kisutu ilikuwa na upungufu wa uchambuzi wa ushahidi dhidi ya washtakiwa.

Jaji Mgeta alisema katika shtaka la kwanza la kula njama, Jamhuri ilishindwa kuthibitisha washtakiwa walikula vipi njama, hivyo mahakama yake imeona kosa la kula njama halijathibitishwa na kuwachia huru washtakiwa.

Katika shtaka la kukusanyika isivyo halali, kufanya maandamano bila kibali na kukaidi amri halali ya Jeshi la Polisi, Jaji alisema siku ya tukio, eneo la viwanja vya Buibui lilikuwa halali kwa wanachama wa CHADEMA kufanya kampeni za wagombea wao.

"CHADEMA walikuwa na mkutano halali katika viwanja vya Buibui na kwamba ushahidi wa Jamhuri umeshindwa kuelezea uhusika wa washtakiwa kufanya mkusanyiko isivyo halali na kutokutii amri ya polisi kutokufanya maandamano na mashahidi wamewatambua washtakiwa wakiwa kizimbani.

"Hakuna shahidi aliyesema nini kilitokea Mwananyamala na kwamba tukio lilitokea muda mrefu lakini mashahidi hawakwenda kutoa taarifa popote wakati lilipotokea.

"Nimeangalia video ya tukio nimeona watu walipotoka viwanja vya Buibui walionekana wakiwa wamenyoosha mikono juu kuonyesha kuwa maandamano yalikuwa ya amani kwa kuwa mawakala walikuwa wanafuata barua tume ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi kesho yake," alisema Jaji.

Kutokana na makosa hayo ya hukumu ya Kisutu, mahakama yake inawaachia huru katika makosa ya kukusanyika isivyo halali, kufanya maandamano na kutotii amri ya polisi ambayo hayajathibitishwa kisheria na kusisitiza kuwa washtakiwa wako huru. Alisema amebaini kuwa Jeshi la Polisi lilichochea vurugu kwa wananchi hao baada ya kupiga mabomu ya machozi na kusababisha mtafaruku.

Alisema Mbowe alikuwa anatoa hoja na malalamiko yake kwamba chama chake na wanachama wananyanyasika namna gani. Alisema mahakama yake inaamuru washtakiwa warejeshewe fedha zao za faini.

Pia alisema pamoja na Dk. Mashini kutokuwa sehemu ya warufani, kwa mujibu wa sheria, ni mnufaika wa hukumu hiyo ameachiwa huru na arejeshewe faini aliyolipa.

Awali upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Faraja Nchimbi akisaidiana na Salimu Msemo, waliwasilisha hoja za kupinga rufani hiyo.

Akijibu hoja za walalamikaji, Wakili wa Serikali Msemo alidai kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba ilizingatia sheria ikiwamo kuchambua ushahidi wa pande zote mbili.

Aliendelea kujibu hoja za rufani, kwamba kuainisha ushahidi inategemea na mwandishi wa hukumu kwa kuwa kila mmoja ana namna yake ya kuandika hukumu, tofauti na Wakili wa walalamikaji Peter Kibatala alivyodai kuwa hukumu imeandikwa kwa kurasa chache.

Alidai kuwa shahidi wa kwanza alieleza mahakamani alivyokuwa akiwasiliana na Dotto ambaye alikuwa eneo la mkutano. Kwa hiyo hakuna chochote kilichopungua upande wa Jamhuri kwa sababu Dotto alikuwepo eneo la tukio tu.

Alidai kuwa kama mahakama itapitia hukumu na mwenendo huu ikaona kwamba kazi ya kuchambua hukumu haikufanyika kikamilifu ikiona upungufu huo, basi inayo mamlaka ya kuvaa viatu hivyo vya Mahakama ya Kisutu na kufanya uchambuzi upya.

Awali Kibatala alidai mahakamani hapo kwamba mahakama ya Kisutu ilikosea kuwapa adhabu Mbowe na wenzake aliiomba Mahakama Kuu itengue hukumu hiyo.

Alidai bila kuacha shaka mashtaka dhidi ya walalamikaji hayakuthitishwa na walalamikiwa hivyo hukumu hukumu hiyo haina mashiko ya kisheria na kudai kuwa mashtaka yote 12 yaliyowatia hatiani washtakiwa hakuna hata moja yaliyochambuliwa kama mwenendo wa mashauri ya jinai unavyotaka kisheria.

Kuhusu ushahidi wa kielektroniki, wakili huyo alidai ushahidi huo ni wa pekee na kwamba ushahidi wowote wa kipekee umewekewa vigezo maalum namna ya kuupokea.

Alidai mahakama ilipaswa kuupokea kupitia ushahidi wa ziada tofauti na ule shahidi anaoutoa akiwa kizimbani ikiwepo kupokewa kwa hati katika mfumo wa hati ya kiapo kama msimamo wa mahakama ya rufaa unavyoeleza.

Katika hoja nyingine, wakili huyo alidai namna hati ya mashtaka ilivyoandaliwa ilikuwa inachanganya kiasi kwamba washtakiwa walishindwa kujua namna ya kujitetea.

Mbali na Mbowe, walalamikaji wengine ni Katibu Mkuu John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu- Zanzibar, Salum Mwalimu, waliokuwa wabunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Esther matiko (Tarime Mjini), Ester Bulaya (Bunda Mjini), Halima Mdee (Kawe), John Heche (Tarime Vijijini).





Rais Samia Suluhu Hassan akimtunza Msanii wa Taarabu, Sabah Salum Muchacho, wakati akitumbuiza katika mkutano wake na wanawake wa Tanzania, jijini Dodoma mapema mwezi huu. Siku hiyo, Rais Samia alitilia mkazo umuhimu wa elimu hasa sayansi na teknolojia kwa watoto wa kike. **PICHA: MAKTABA**

# Kila kukicha anazidi kuinoa sekta mama ya elimu nchini

- Rekodi Afrika wajawazito kurudi darasani
- Kawafuta machozi wadaiwa elimu ya juu
- Ajipanga 'LY' wa elimu bure mwakani

**Na Christina Mwakangale**

UNAPOZUNGUMZA kuhusu wanawake walioingia kwenye rekodi mpya duniani, hutaacha kumtaja Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na kuwa miongoni mwa marais wachache wanawake duniani.

Katika mfululizo wa makala za kuelekea siku 100 za mwanzo za uongozi wake zinazotimu kesho, leo tunaiangazia Sekta ya Elimu.

Ndani ya muda huo wa miezi mitatu na theluthi, Rais Samia ameonekana kuwa na nia ya kuiinua sekta hiyo muhimu kwa kuipa kipaumbele kibajeti na kuyakumbuka makundi yaliyokuwa yameachwa nyuma, hasa watoto wa kike.

### MTAALA KUFUMULIWA

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeweka wazi kwamba ndani ya uongozi wa Rais Samia, itahakikisha inafumua mtaala wa elimu nchini ili kuzalisha wahitimu wenye sifa zinazohitajika katika soko la ajira na wenye uwezo wa kujiajiri na kuajiri wenzao.

Wiki iliyopita kulifanyika kongamano la kwanza za utekelezaji wa kusudio hilo mgeni rasmi akiwa ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako.

Prof. Ndalichako ambaye ni mtaalamu wa mitaala, alisema serikali imesikia kilio cha Watanzania na kuamua kuboresha elimu nchini kwa kuanza kukusanya maoni ya kuboresha mtaala wa elimu kuanzia ngazi ya msingi. Mabadiliko hayo ni ya sita nchini.

### ELIMU BURE

Aprili mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti kuhusu ubashiri wa kitakwimu unaoonyesha kutakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Mtazamo huo ulizingatia ukweli kwamba kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaoandikishwa kujiunga na shule za msingi nchini tangu mwaka 2016, serikali ilipoanza kutekeleza Mpango wa Kutoa Elimu Bila Malipo, maarufu Elimu Bure.

Serikali ya Rais Samia kwa kulitambua hilo, imeamua kuongeza bajeti ya ziada ya Sh. bilioni 125 ili kuanza ujenzi wa maboma ya madarasa 10,000 kwa ajili ya kuwachukua wanafunzi hao.

### WENYE UJAUZITO DARASANI

Serikali ya Rais Samia pia imetangaza kuwaruhusu wanafunzi waliokatiza masomo yao kutokana na kupata ujauzito, kurejea masomoni kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, akizungumza na wakuu wa vyuo vya maendeleo ya wananchi hivi karibuni, amewataka wakuu hao wa vyuo kuhakikisha wanafunzi wa kike walioshindwa kuendelea na masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, warudi na kuendelea na masomo.

Aliwataka wakuu hao wa vyuo kutekeleza agizo hilo la kudahili wanafunzi hao kuanzia mwakani.

Pia, aliagiza vyuo vyote vya maendeleo ya wananchi viwe vimesajiliwa kama vituo vya kufanyia mitihani ya kidato cha pili na nne.

Aliweka wazi kuwa hatua hiyo ya kurejesha wanafunzi wa kike waliokatiza masomo yao inatokana na majadiliano ya muda mrefu kati ya wizara na Benki ya Dunia (WB).Alisema wanafunzi hao watarejea darasani kuanzia mwakani katika vyuo 54 wasichana waliokatiza masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba kupata haki ya elimu.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandikia barua WB kuishauri kusitisha kuikopesha Tanzania Dola milioni 500 kwa ajili ya uboreshaji wa elimu kutokana na kuzuia wanafunzi waliopata mimba, kurejea shuleni.

### KICHEKO ELIMU YA JUU

Katika kufanikisha elimu ya juu, serikali ya Rais Samia imelazimika kuongeza Sh. bilioni 70 kwenye bajeti ya iliyokuwa imetengwa ya Sh. bilioni 500 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka ujao wa masomo.

Lengo ni kuhakikisha wanafunzi wote wenye sifa za kupata mkopo, waliokosa kutokana na ufinyu wa bajeti, wanapata mikopo hiyo.

Waziri wa fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akihitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, aliliambia Bunge wiki hii kuwa wamezungumza na Prof. Ndalichako ili wanafunzi 11,000 waliokosa mkopo mwaka jana na 10,000 mwaka huu wapate mkopo.

"Bajeti hii ya Sh. bilioni 464 kwa 2020/21 imeongezeka kutoka Sh. bilioni 450 mwaka 2019/20 ambazo zinawanufaisha jumla ya wanafunzi 132,119," alibainisha.

### MAKATO YA KINYONYAJI

Ndani ya muda mfupi tangu aapishwe kuwa Rais wa Tanzania Machi 19 mwaka huu, Rais Samia amefuta kilio cha muda mrefu kilichosikika kuhusu kile kilichotangazwa kuwa unyonyaji katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Makato yaliyokuwa yanalalamikiwa na wanufaika wa mikopo hiyo inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ni pamoja na penalti ya asilimia 10 ya mkopo kwa mnufaika anayeshindwa kuanza kurejesha mkopo baada ya kumalizika kwa kipindi cha neema cha miaka miwili baada ya kuhitimu masomo yake.

Mengine ni tozo ya asilimia moja ya mkopo kwa ajili ya uendeshaji wa bodi ambayo watumishi wake wanalipwa mishahara na stahiki zinginezo na serikali.

Pia utaratibu wa deni kuongezeka kwa asilimia sita (6) ya mkopo kila mwaka kuanzia tarehe ambayo mnufaika alianza kupokea fedha.

Suala la nne lililolalamikiwa ni uamuzi wa serikali kufanya marekebisho ya kisheria na kuanza kukata asilimia 15 ya mshahara wa mnufaika kila mwezi kutoka asilimia nane (8) ya awali.

Katika hoja hizo nne, Rais Samia amekubaliana na hoja mbili za kufuta utaratibu wa 'riba' ya asilimia sita kila mwaka na penalti ya asilimia 10 ya mkopo.

### AJIRA ZA WALIMU

Chini ya uongozi wa Rais Samia, serikali imetenga Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi, wakiwamo walimu.

Vilevile serikali imetenga Sh. bilioni 200 kwa ajili ya kuajiri watumishi 40,000 katika Sekta za Afya, Elimu, Ardhi na Kilimo.

### KUPANDISHWA MADARAJA

Mwezi huu maelfu ya watumishi wameshuhudia kupandishwa kwa madaraja yao na hivyo kuwa na ongezeko kwenye mishahara yao.

Serikali chini ya Rais Samia, imetenga Sh. bilioni 499 kwa ajili ya upandishwaji wa madaraja, kwa mujibu wa waziri mwenye dhamana ya utumishi, Mohamed Mchengerwa.

# Mbaroni tuhuma kumuua shangazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia kijana kwa tuhuma za kumuua shangazi yake kwa kumcharanga mapanga akimtuhumu kuwa ni mchawi na amekuwa akimroga asipate maendeleo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei alimtaja aliyeuawa kuwa ni Lamina Samwebe (65), mkazi wa Ngamanga Misheni katika Kata ya Ipinda wilayani Kyela.

Alisema jina la kijana huyo limehifadhiwa kwa sababu za kiusalama na anadaiwa kufanya mauaji hayo Juni 22 mwaka huu kwa kumvamia shangazi yake huyo akiwa amelala nyumbani kwake saa 5:45 usiku kisha akatekeleza unyama huo.

Alisema kijana huyo alimkata na panga shangazi maeneo ya kichwani, shingoni na vidole vitatu vya mkono wa kulia na kwamba bibi huyo alikosa msaada kutokana na kuishi peke yake kwenye nyumba hiyo.

"Baada ya kupata taarifa, askari walifika katika eneo la tukio na kukuta shangazi yake akiwa amekufa chumbani kwake, walipofuatilia walimkuta kijana huyo akiwa na panga ambalo alilitumia kwenye mauaji hayo na ndipo wakamtia mbaroni," alisema Kamanda Matei.

Alisema kijana huyo bado anashikiliwa wakati upelelezi wa tukio hilo ukiendelea ili kumfikisha mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria na kwamba mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Kituo cha Afya cha Ipinda.

Kamanda Matei aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Aliwataka wale ambao wanaona kuwa wanatendewa ndivyo sivyo, kufika kwenye vyombo vya kisheria kutoa taarifa ili hatua zichukuliwe badala ya kujichukulia sheria mkononi, jambo ambalo ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria.

Vilevile, aliwataka kuachana na dhana potofu za imani za kishirikina kwa maelezo kuwa zimepitwa na wakati na kwamba zimekuwa zikisababisha migogoro katika jamii na wakati mwingine kusababisha maafa miongoni mwa wanajamii.

"Haya mauaji yamekuwa yakiongezeka kwenye jamii, sasa tutawaomba wazee wetu wa mila watusaidie kutoa elimu kwa wananchi ili kuondoa imani hizi zilizopitwa na wakati, lakini wazee hawa watatusaidia kuwafichua waganga wanaopiga ramli chonganishi," alisema Kamanda Matei.

Alisema jeshi hilo litaendesha msako maalum wa kuwasaka waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi na kuwachukulia hatua za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo.




Meneja wa Benki ya DTB Tawi Kuu la Dar es Salaam, Shahista Adam (wa pili kushoto), akimkabidhi vifaa vya kujifungulia Zuhura Msangi katika Kituo cha Afya Buguruni jana. DTB kwa kushirikiana na Klabu ya Rotary ya Masaki (RCM), wametoa msaada wa vifaa 450 kwa hospitali za Mbagala Rangi Tatu, Kigamboni na Buguruni, kwa ajili ya kusaidia wajawazito wakati wa kujifungua. Kutoka kulia ni Ofisa Muuguzi wa Jiji la Dar es Salaam, Gerwalda Mumba, Rais wa RCM, Ashna Tanna na Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa DTB, Jesca Tugara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwongozo wa tiba wazingatia corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa matibabu nchini na orodha ya taifa ya dawa muhimu, ukizingatia matibabu ya ugonjwa mpya wa corona.

Vilevile, katika kuimarisha huduma za afya nchini, dawa mpya 101 zimeongezwa katika orodha hiyo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo jijini hapa jana, alipozindua mwongozo huo ambao umeandaliwa na wizara yake kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Wadau walioshiriki ni pamoja na vyama vya kitaaluma na wadau wa maendeleo ikiwamo Mradi wa HPSS Tuimarishe Afya unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi.

Alisema mwongozo huo umepitiwa ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na kitabibu na mabadiliko ambayo yameainishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa kulingana na utafiti mbalimbali.

"Mwongozo huu umepitiwa kukidhi maboresho ya huduma za matibabu katika ngazi ya msingi au kukidhi kupanuka kwa huduma za kibingwa na kutoa mwongozo wa kutibu magonjwa mapya yanayoibuka.

"Mabadiliko muhimu katika toleo hili la sita ni pamoja na kutoa mwongozo juu ya menejimenti na matibabu ya ugonjwa mpya wa COVID-19, ambayo yametolewa ufafanuzi katika sura ya magonjwa ya mlipuko.

"Aidha, imeandaliwa sura mpya ya jinsi ya kuwahudumia wagonjwa wa dharura," alisema.

Kuhusu orodha mpya ya dawa, Dk. Gwajima alisema baadhi ya dawa zimeongezwa ili kukidhi maboresho ya huduma za kibingwa katika kupandikiza figo.

Alisema katika kuimarisha huduma za afya ya msingi dawa zimeshushwa kutoka ngazi ya hospitali za wilaya hadi vituo vya afya ili kuboresha huduma za mbalimbali ikiwamo za upasuaji.

"Dawa hizo ni pamoja na zinazotumika katika upasuaji, shinikizo la damu na zile za kutibu kisukari," alisema.

Waziri huyo alisema katika mwongozo huo daktari bingwa anaruhusiwa kuandika dawa zote zilizopo kwenye mwongozo kulingana na eneo lake la kitaaluma bila kuzingatia ngazi anayofanyia kazi.

Alisema orodha hiyo ya dawa muhimu itaendelea kutumiwa na Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) kulingana na sheria huku akiagiza kamati za dawa na tiba katika ngazi zote kusimamia matumizi sahihi ya dawa kulingana na mwongozo huo.

Awali, Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifell Sichwale, alisema mchakato wa kuandaa mwongozo huo ulianza Desemba 2019 na umezingatia mabadiliko ya teknolojia na utengenezaji wake umeshirikisha wataalamu wa afya.

# Wageni kupata vibali vya kazi ndani ya saa 24

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema imekamilisha mfumo wa maombi ya vibali vya kazi kwa njia ya kielektroniki kwa wageni ambavyo sasa vitatolewa ndani ya saa 24.Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), William Ole Nasha, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano mkuu wa 62 wa mwaka wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Ole Nasha alisema serikali imefanya utoaji wa vibali hivyo kuwa rahisi kwa kuanzisha mfumo huo ili kupunguza gharama za kuvipata.

"Hii ni sehemu ya kupunguza na kuondosha vikwazo vya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi kuja Tanzania," alisema.

Alisema serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kazi na wafanyakazi kwa kusimamia viwango vya kazi na wafanyakazi pamoja na afya na usalama mahali pa kazi.

"Hadi Februari, mwaka huu jumla ya kaguzi 4,771 za viwango vya kazi zimefanyika sawa na asilimia 99.4 ya kaguzi 4,800 zilizopangwa kufanyika. Kaguzi 110,123 zimefanyika zilizohusu afya na usalama mahali pa kazi, serikali imefanya juhudi hizi kuhakikisha hata wawekezaji wanapokuja kuwekeza watafanya hivyo katika mukhtadha wa sheria za kazi ambazo ni rafiki kwa wafanyabiashara," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema mkutano huo umebebwa na mada kuu isemayo, "Kuimarisha uwekezaji na mazingira ya biashara Tanzania kwa ajili ya uchumi wa kiushindani na ajira endelevu.

**Summons to appear (O.V.R.20 (1)(CPC)**
**(SUBSTLTUTED SERVICES)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**LAND DIVISION**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO.24 OF 2021**

**DR.JULIUS MASSAGA ……………………………………PLAINTIFF**
**VERSUS**
**VIGUTA LIMITED………………………………………………1st PLANTIFF**
**CHRISTINA RWEBANGIRA…………………………………2nd PLANTIFF**
**SALMIN IBRAHIM DAUDA…………………………………3rd PLANTIFF**

**TO. VICOBA LIMITED**
**VIGUTA,NKURUMAH STREET**
**PLOT NO.2035/155,**
**CLOCK TOWER BUILDING 3rd FLOOR**
**P O BOX 95033,**
**DAR ES SALAAM**

**CHRISTINA RWEBANGIRA**
**CAG HEADQUARTERS,**
**UKAGUZI STREET,**
**P O BOX 950,**
**DODOMA**

**SALMIN IBRAHIM DAUDA**
**CAG HEADQUARTERS,**
**UKAGUZI STREET,**
**P O BOX 950,**
**DODOMA**

**WHEREAS** the above named plaintiff has instituted a suit against you.you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 14th july,2021 at 10:00 am to answer the claim.and you are directed to bring any document which you wish to rely in support of your defence.

**TAKE NOTICE** that,in default of your appearance on that before mentioned ,the suit will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court,this…..18th day of june 2021.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT LAND DIVISION

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji kuweni makini kipindi hiki cha usajili

**LIGI** Kuu ya Tanzania inaelekea ukingoni huku kila timu ikiangalia na kufanya tathmini ya kile ilichovuna kuanzia mwanzo wa mashindano hadi walipofika hivi sasa.

Timu zinafanya tathmini ya kujua kama wamefanikiwa kufikia malengo waliyoyaweka kabla ya kuanza kwa msimu huo au la.

Ikiwa wamefikia malengo ni jambo la kheri lakini kama wameshindwa waangalie wapi walipojikwaa na kurekebisha baadhi ya makosa waliyofanya ili yasijirudie katika msimu ujao wa ligi.

Sio kwamba dirisha la usajili limefunguliwa la hasha bali ni kutokana na baadhi ya wachezaji ambao mikataba yao imefika mwishoni au walio na mikataba chini ya miezi sita ambao kikanuni wanaruhusiwa kufanya mazungumzo na timu nyingine.

Katika madirisha ya usajili mara nyingi kumekuwa na utata hasa kwa wachezaji kusaini timu zaidi ya moja tuliwahi kuona kwa nyota kama winga Mrisho Ngasa mwaka 2013 wakati akijua fika ana mkataba na Azam FC, lakini alisaini mkataba wa siri na Yanga jambo lililomfanya apigwe faini ya Sh. milioni 45 kwa kosa hilo.

Kiungo mshambuliaji Mohamed Mkopi mwaka 2016 alijikuta akikaa nje ya uwanja mwaka mzima baada ya kusaini timu mbili wakati akijua fika bado hajamalizana na waajiri wake Tanzania Prisons, akasaini kwa watani wao wa jadi Mbeya City jambo lililomfanya akutane na rungu hilo.

Pius Buswita, ambaye alidumu katika kikosi cha Yanga kwa miaka miwili wakati anaondoka Mbao aliingia kandarasi na Simba, lakini baadaye akasaini Yanga, jambo ambalo likamfanya apitiwe na rungu la kufungiwa na kutakiwa kurudisha fedha za Simba.

Naye kiungo wa zamani wa Kagera Sugar, Ludovic Venance mwaka 2017 alipitiwa na rungu baada ya kusaini mkataba mpya na African Lyon, wakati akijua fika kuwa bado ni mwajiriwa wa Mbao FC, ambapo alijikuta akikosa michezo minne ya timu yake mpya.

Sakata kama hili pia limetokea msimu wa 2020/21 ambapo kiungo Benard Morrison, amesaini kandarasi na Simba wakati klabu ya Yanga ikidai kuwa ina mkataba na mchezaji huyo ambapo hadi sasa kesi ya wawili inaendelea katika Mahakama ya Usuluhishi (CAS).

Wakati tukisubiri shirikisho la mpira wa miguu hapa nchini kutangaza tarehe ya ufunguzi wa dirisha la usajili, Nipashe tunatoa rai kwa wachezaji pamoja na klabu kuwa makini kipindi hiki ili kukwepa kukutana na adhabu za kufungiwa na kulipishwa faini kwa kosa ambalo limekuwa likijirudia misimu nenda rudi.

Tunaamini timu pamoja na wachezaji watajifunza kupitia kwa mifano hii ambayo iko wazi ili kulinda taswira ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na wao katika jamii ya wapenda soka.

Pia tunatoa angalizo kwa klabu nazo zinatakiwa kuwa makini kwenye sajili zake, katika kuhakikisha kwamba, mchezaji wanayemsajili hajafanya hivyo kwa timu nyingine.

Klabu zinatakiwa kuhakikishe wachezaji ambao wanawasajili wanakuwa hawajaingia kwenye makubaliano na timu nyingine ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza kwa kuanza kupelekana kwenye vyombo vya sheria.


Nalo Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, linatakiwa kuwa makini wakati wanapopelekwa orodha ya wachezaji ambao wamesajiliwa na timu husika, katika kuhakikisha jina la mchezaji mmoja halijitokeze katika timu mbili.

Kama wahusika wote, wachezaji, klabu na TTF watatimiza majukumu yao vizuri, Nipashe tunaamini kwa suala hili halitaweza kujitokeza kwa mchezaji mmoja kujisajili kwenye timu mbili tofauti.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Chako ni chako cha mwenzako...

Na barnabas Maro

**NAAM!** (tamko linalotumika kwa kuitikia; = labeka!, ndio!, taib!) kwa maana wahenga walisema "chako ni chako, cha mwenzio si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

Methali hii yatufunza tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine. Pia yatukumbusha kuthamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama watu wengine.

Mpaka sasa timu zetu zinazoshiriki Ligi Kuu nchini, hasa Simba na Yanga zinakazana kusajili wachezaji kutoka mataifa mengine n-nje ya Tanzania ambao hulipwa mishahara mikubwa zaidi ya wachezaji wetu wa nyumbani!

Laiti timu zetu zingetambua kuwa " Nguo ya kuazima haistiri (haifichi) makalio, wangejibidiisha kuwa na utaratibu wa kuziandaa timu zao kwa kupata walimu mahiri, hata kutoka ughaibuni ili kuwafunza vijana wa umri kuanzia miaka 12 mpaka 20. Hawa wangepelekwa hata shule za n-nje kupambana na vijana wenzao huko ughaibuni ili kujikomaza zaidi.

Yafaa timu zetu zitambue kuwa nguo ya kukopa au kuazima haiwezi kuyaficha makalio ya mtu vizuri kwani badala yake yaweza kumwaibisha. Methali hii hutumiwa kutunasihi tusipende vitu vya kuazima kwa kuwa wanaotuazima vitu hivyo waweza kutuaibisha.

Kama timu zetu haziwezi kuwa na utaratibu huu, basi TFF ianzishe shule itakayokuwa na walimu wa kigeni ili kuwafundisha wenyeji jinsi ya kufunza vijana namna bora na sahihi ya uchezaji.

> **Kama timu zetu haziwezi kuwa na utaratibu huu, basi TFF ianzishe shule itakayokuwa na walimu wa kigeni ili kuwafundisha wenyeji jinsi ya kuwafunza vijana namna bora na sahihi ya uchezaji.**

Tukiwa na shule za kuwafunza walimu wetu wenyewe ili kuepuka usajili wa walimu wa kigeni itakuwa bora zaidi.

Mambo haya yakitimizwa, timu zetu zitaokoa fedha nyingi zinazotumika kuwalipa walimu na wachezaji wa kigeni waliosajiliwa na timu mbalimbali humu nchini. Vinginevyo tutaendelea kuwategemea wageni huku fedha zetu adimu (-enye kupatikana kwa uchache au shida) zikiwanufaisha wanaosajiliwa kutoka n-nje ya nchi!

Jambo lingine ni uwepo wa viwanja visivyokidhi mchezo wa kandanda kama alivyoelekeza Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni. Vinavyostahiki kuitwa viwanja bora vya kandanda humu nchini ni vichache mno. Ukiondoa viwanja vya Uhuru, Benjamini Mkapa na Azam Complex vilivyopo Dar es Salaam na kile cha Kagera Sugar, vilivyobaki vinatia aibu!

Cha kushangaza ni kwamba viwanja vilivyobaki nchini vinatia aibu ingawa vilitwaliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kama vilifanyiwa maendeleo na chama hicho, basi ni 'maendeleo' ya kuvipaka rangi ya kijani na njano kisha kuandikwa maneno ya kukisifu chama hicho.

Bila kujali kuwa viwanja hivyo ni 'mali' ya CCM, serikali iliyo madarakani yapaswa kukabidhi viwanja hivyo kwa vyama vya mpira vya mikoa husika au mikoa hiyo ili vitengenezwe upya na kutunzwa vizuri kama itakiwavyo. Jambo hili pia laweza kujadiliwa Bungeni ili kuilazimisha CCM kuvitengeneza viwanja hivyo kama itakiwavyo au kuvikabidhi kwa mikoa husika. Itapendeza kama kila mkoa utakuwa na uwanja mzuri wa kisasa kwani kwa kuwa na viwanja vizuri vinavyotunzwa huenda mashindano ya kandanda kugombea Kombe la Dunia ikafanyika Tanzania yenye vivutio vingi vya utalii visinyokuwapo nchi nyingi duniani.

"Mwenye moyo wa kuonywa huonywa." Maana yake anayesikiliza na kuyafuata mashauri anayopewa hufaidika. Twafunzwa tuwe na tabia ya kusikiliza na kufuata mashauri tunayopewa na wanaotuzidi ujuzi au maarifa ili tusijefikwa na maafa au majuto baadaye.

Kadhalika "Mwenye busara mara hunasihika." Mtu mwenye hekima hufuata ushauri apewao. Hutumiwa kutukumbusha umuhimu na faida za kuyafuata mashauri tupewayo.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (kushoto), akisalimiana na Mzee Augustino Sambagi, baada ya kumaliza mkutano na wazee wa Manispaa ya Iringa juzi, kwa ajili ya kusikiliza kero zao mbalimbali. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mbaroni tuhuma kujifanya RCO

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Masanja Maduhu (49) mkazi wa mkoani Simiyu, kwa tuhuma za kujifanya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa (RCO) wa Shinyanga na kujipatia Sh. 200,000 kutoka kwa mfanyabiashara Hilali Soud.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa wiki iliyopita na anashikiliwa na polisi.

Alisema upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akijipatia fedha mara kwa mara kwa udanganyifu na kujifanya ofisa wa Jeshi la Polisi.

Kamanda Kyando alisema Desemba 20, mwaka jana, Maduhu alijifanya ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa (RTO) na kujipatia fedha Sh. 100,000.

"Mtuhumiwa huyu alimtapeli fedha mfanyabiashara Hillali Soud kwa kumlaghai ampatie Sh. 200,000 ili aweke mafuta kwenye gari la polisi na Sh. 100,000 alimtapeli mwananchi mmoja, Hamisi Ally, ambaye baadaye aliandika barua ya kufuta mashtaka na mtuhumiwa akaachiwa huru," alisema Kyando.

"Baada ya kuachiwa huru mtuhumiwa ameendelea tena na tabia yake ya kutapeli watu kwa kutumia mwavuli wa Jeshi la Polisi kinyume cha sheria na kutuchafua. Tutamfikisha mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili baada ya upelelezi kukamilika," aliongeza.

# Wasafirishaji wanalilia serikali

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa usafirishaji, ikiwamo Chama cha Wamiliki wa Malori (TATOA) na Mawakala wa Forodha (TAFFA), wameiomba serikali kufikisha kilio chao kwa Chombo cha Kisheria Zambia (SI), kufanyia marekebisho muswada wa sheria ambao utaruhusu mizigo inayopitia Bandari ya Dar es Salaam kubebwa na raia wa Zambia pekee.

Muswada huo wa Sheria wa Uwezeshaji Wananchi Usafirishaji wa Mizigo Mizito kwa Pamoja kwa Njia ya Barabara Mwaka 2021, utaruhusu mizigo kupitia bandari hiyo kwa asilimia 50 kubebwa na Wazambia, asilimia 30 ibebwe na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na iliyobaki ibebwe na malori kutoka Tanzania.

Makamu Mwenyekiti wa TATOA, Elias Lukumay, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema sheria hiyo ikianza kutumika itaathiri uchumi wa Tanzania hususani madereva wa malori pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema sheria hiyo itawanyima haki ya ushindani kibiashara usio na uwiano na wameandika barua kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa pamoja na Waziri wa Uchukuzi ili kufikisha ujumbe wao Zambia.

"Tunajua Zambia inakaribia kufanya uchaguzi mkuu, tutasubiri marekebisho haya lakini ifahamike hili suala ni la dharura, sekta ya usafirishaji imeajiri wengi na ni ya kwanza katika kuchangia fedha za kigeni na kwenye uchumi wa nchi inachangia asilimia nane ya Pato la Taifa.

"Muswada ukipitishwa, Tanzania haitafikia matarajio ya tani milioni 30 kwa mwaka bandarini licha ya maboresho ya hivi sasa ya upanuzi wa barabara, kuongeza kina katika gati na miundombinu mingine," alitahadharisha Lukumay.

Pia alisema muswada huo utainyima Tanzania mapato ambayo hutokana na malori ya kubeba mizigo kupitia mafuta ambayo hutumia lita milioni mbili kwa ajili ya kufanya safari za Tanzania - Zambia.

Katibu Mtendaji wa TAFFA, Elitunu Malamia, alisema sekta binafsi ni wadau wa maendeleo ambao hushirikiana na serikali katika kufikia malengo kiuchumi.

"Asilimia 70 ya mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam inakwenda SADC. Zambia ni nchi ya pili katika kupitisha mizigo bandari hii ikitanguliwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Muswada huu ukipita, utatuathiri Watanzania, tusiruhusu usafirishaji wa mizigo uwe wa kugawana mizigo kusafirisha," alisema Malamia.

# Ataka urasimu uondolewe uwekezaji umeme

**Na Faustine Feliciane**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto, ameiomba serikali kuondoa urasimu katika uwekezaji kwenye sekta ya nishati ili kuruhusu wawekezaji binafsi.

Akizungumza jana kwenye semina juu ya matumizi ya taka kuwa nishati ya umeme, iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Kumbilamoto alisema kuna kampuni ambazo zinataka kuwekeza kwenye sekta hiyo lakini zinakumbana na vikwazo mbalimbali.

"Mkoa wetu unawahitaji sana wawekezaji katika sekta hii kwa sababu Dar es Salaam ina zaidi ya wakazi milioni sita na tunazalisha taka tani 4,600 hivyo kama kampuni inakuja kuwekeza katika teknolojia hii ya kubadili taka kuwa umeme itakuwa faida kubwa sana. Mkoa utakuwa safi lakini pia umeme utakuwa mwingi, hivyo hata bei itashuka," alisema Kumbilamoto.

Pia alisema manispaa zote za Dar es Salaam ziko tayari kuwakaribisha wawekezaji kama hao lakini kunakuwa na urasimu serikali kuu.

"Naongea haya watu wa TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) wapo hapa. Ni vyema basi wakaona namna ya kuingia ubia na kampuni kama hizi ambazo zinatumia taka kuzalisha umeme," alisema.

Kauli hiyo iliungwa pia mkono na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud ambaye alisema Zanzibar kwa ujumla wake inahitaji sana umeme wa uhakika kutokana na kuwapo kwa fursa nyingi za uwekezaji hususan kwenye utalii kwa ujenzi wa hoteli.

"Hii teknolojia ikifika Zanzibar na kuruhusu wawekezaji itasaidia sana Zanzibar kuwa na umeme wa uhakika ambayo hatutautegemea kutoka popote kwa kuwa utakuwa unazalishwa Zanzibar," alisema.

Pia alisema kisiwa cha Unguja kinategemea umeme kutoka Dar es Salaam huku kisiwa cha Pemba kikitegemea zaidi umeme kutoka mkoani Tanga.

Semina hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na wataalamu kutoka TANESCO, iliandaliwa na kampuni ya Eco-Waste Holdings ya Uswisi huku ikifadhiliwa pia na ubalozi wa nchi hiyo hapa nchini.

Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chassot, alisema ujio wa kampuni hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya nchi hiyo na Tanzania katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Alisema kuwa Uswisi itaendelea kusaidiana na serikali ya Tanzania ili kufikia malengo ya maendeleo iliyojiwekea.

# Utelekezaji familia kikwazo maendeleo

**Na Elizabeth Zaya**

UTELEKEZAJI wa familia na unyanyapaa kwa wanawake vimetajwa kuwa miongoni mwa vikwazo kwa kundi hilo kimaendeleo.

Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dotto James, alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipofungua mafunzo kwa wanawake wajasiriamali kutoka Tanzania Bara na Visiwani yaliyoandaliwa na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EQTF) ikiwa ni maandalizi ya kuelekea maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara (DITF), maarufu Sabasaba.

Alisema pamoja na mwamko uliopo kwa sasa kwa wanawake wengi kufanya shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato, bado wamekuwa wakikwamishwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo wengi wao kunyimwa haki zao za msingi na utelekezaji wa familia.

"Matukio haya yote yanaenda kinyume cha Sera ya Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2000.

"Ni jukumu letu sote kuweka mikakati ya kuhakikisha wanawake wote bila kujali hali zao, wanapata haki zao zote za msingi kwa ajili ya kuleta maendeleo chanya katika uchumi wa viwanda," alisema James.

Aliongeza kuwa ipo haja kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika shughuli za maendeleo na uzalishaji kutokana na uwezo wao mkubwa wa kubaini na kutumia rasilimali katika kujiongezea kipato na kuondoa umaskini katika familia na kwenye jamii.

"Kwa hiyo kuanzia katika ngazi ya familia hadi serikali kuu, tunatakiwa kuwawezesha wanawake ambao wengi wao ndiyo wazalishaji katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini kwenye viwanda vidogo na sanaa za mikono, kuendelea kuwaunga mkono ikiwamo kuwapatia elimu elekezi ili wafike mbali zaidi.

"Wanawake ni kundi muhimu katika jamii, hivyo wanapaswa kupewa kipaumbele katika kuwawezesha kielimu, kisiasa na kiuchumi kwa ujenzi wa taifa lenye uhakika na mafanikio," alisema.

Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, Anna Mkapa, alisema mafanikio yote ya kijamii, kiuchumi na elimu yanatokana na mchango wa mwanamke.

"Na ndiyo maana tukaona kwamba kuna umuhimu kwa kuendelea kuwashika mkono wanawake hawa wanaopambana kuinua uchumi wa familia, jamii na nchi kwa ujumla kwa kuwapa elimu ya fursa mbalimbali na namna ya kuzitumia.

"Niombe jamii iendelee kuwaamini na kutambua umuhimu wao," alisema Anna.

# Wanawake watajwa wizi simu minadani

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

IMEDAIWA kuwapo wimbi la wanawake wanaojihusisha na wizi wa simu katika minada mbalimbali mkoani Shinyanga kunakosababisha wengi wao kushindwa kufanya shughuli halali.

Mwekahazina wa Wajasiriamali mkoani Shinyanga, Seleman Mwarabu, aliwasilisha kilio hicho kwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alipotembelea Mnada wa Tinde wilayani Shinyanga kwa ajili ya kuhamasisha usafi na kuchukua tahadhari dhidi ya corona.

"Mkuu wa wilaya, katika minada hii tunasumbuliwa na kundi la wanawake ambao wanajihusisha na wizi. Ninapoongea na wewe sasa hivi, tayari mfanyabiashara mmoja ameibiwa simu mbili asubuhi hii," alidai.

Mwarabu alisema yeye mwenyewe alishawahi kuibiwa nguo kwenye mnada huo baada ya kwenda kutafuta chenji, kumbe kulikuwa na wanawake waliokuwa wametegesha maeneo hayo, alipotoka tu waliweka nguo ndani ya nguo walizovaa na kutoweka.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Mboneko, aliwataka wafanyabiashara kwenye minada, wawe makini na mali zao kutokana na mwingiliano wa watu wengi.

Aliwataka wachukue tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa kuweka ndoo za kunawa mikono kwenye biashara zao pamoja na kuvaa barakoa.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe (kulia), baada ya kuwasili katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo, mkoani humo juzi, kwa ajili ya kuwakutanisha pamoja wafanyabiashara na kubadilishana nao mawazo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi BRELA wachangia damu Amana

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa Wakala wa Usajili, Biashara na Leseni (BRELA) wamechangia damu na kukabidhi mahitaji mbalimbali kwa wagonjwa katika Hospitali ya Rufani ya Amana, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyomalizika wiki hii.

Aidha, wametumia fursa hiyo kufanya usafi na kuwapatia elimu juu ya huduma za usajili wa biashara na leseni kwa wafanyabiashara katika Soko la Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili wakati wa kukabidhi mahitaji hayo jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka BRELA, Rhoida Andusamile, alisema hatua hiyo imefikiwa ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo ilianza Juni 16 na kilele chake kufikia Juni 23, mwaka huu.

Alisema watumishi wa BRELA walikabidhi mahitaji mbalimbali ya wagonjwa ikiwa wa hospitali hiyo ambayo ni pamoja na sabuni, taulo za kike (pads) na diapers za watoto na wakubwa.

Mkuu huyo alisema taasisi hiyo pamoja wa kuwezesha biashara kwa kusajili majina ya biashara, kampuni, alama za biashara na huduma, utoaji wa leseni za biashara kundi A na leseni za viwanda, inajali jamii inayoizunguka kwa kuwapatia msaada pindi fursa inapopatikana.

"Ndiyo maana BRELA imefika Hospitali ya Amana na kuchangia mahitaji ya msingi ya wazazi na watoto ili wanapoendelea na matibabu wawe katika hali ya usafi," alisema Andusamile.

Aliongeza kwamba utaratibu huo utaendelea kufanyika katika hospitali mbalimbali za hapa nchini. Akipokea msaada huo, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama Dk. Baya Kissiwa, aliishukuru BRELA kwa msaada ilioutoa kwa wagonjwa na kutoa wito kwa taasisi zingine kufika hospitalini hapo na kuwasaidia wagonjwa.

Dk. Kissiwa alisema hospitali hiyo kwa sasa ina uhitaji mkubwa wa damu hasa kwa wazazi wanaofika hospitalini hapo kwa matibabu, hivyo inawaomba wananchi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Kwa upande wa Soko la Kisutu, watumishi wa BRELA walitoa elimu kwa wafanyabiashara na kuwahimiza kufanya sajili za biashara ili kuzipa utu wa kisheria biashara zao.

Pamoja na kutoa elimu sokoni hapo, watumishi wa BRELA walifanya usafi ndani ya soko hilo, ikiwa ni moja ya jukumu la watumishi wa umma kuwajibika kwa wananchi.

Awali, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Seka Kasela, alitumia Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kuwahudumia wateja waliofika katika ofisi za BRELA kupata huduma mbalimbali.

Maadhimisho haya yanayoratibiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yalifanyika kaulimbiu ikiwa ni "Kujenga Afrika Tunayoitaka, Kupitia Utamaduni wa Uadilifu Ambao Unastawisha Uongozi Wenye Maono hata Katika Mazingira ya Mgogoro."





Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Prof. Godius Kahyarara (kulia), akikabidhi mwongozo wa uwekezaji kwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alipotembelea makao makuu ya CCM Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ma - RAS, wakurugenzi wapewa kibarua kizito

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha vifaa vya maabara kwa shule za sekondari na msingi na vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu vinapelekwa kabla ya Julai 15, mwaka huu.

Vifaa hivyo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.4 vimenunuliwa na serikali ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014.

Akizungumza katika uzinduzi wa ugawaji na usambazaji wa vifaa hivyo jana jijini Dodoma, Naibu Waziri,Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema vifaa hivyo vimenunuliwa kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) na Mpango wa Kuimarisha kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LENS).

Silinde alisema vifaa vya maabara vitagawanywa kwa shule za sekondari 1,253 na kutumika katika maabara za Fizikia, Kemia na Biolojia na vifaa saidizi vitapelekwa shule 697 za msingi na sekondari ili kuimarisha uoni, uwezo wa kujongea, usikivu, kujikinga na mionzi hatarishi ya jua kulingana na uleamvu wao.

Alibainisha kuwa ununuzi wa vifaa hivyo ni jitihada za serikali katika kuongeza ushiriki wenye tija wa wanafunzi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji.

"Pia makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi hakikisheni mnawasilisha taarifa ya mapokezi na usambazaji wa vifaa hivi kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kabla ya Julai 20, mwaka huu,"alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leornad Akwilapo, alisema vifaa hivyo vimegaiwa ili kutoa fursa ya kupata elimu kwa muda wote.

Awali, Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, alisema vifaa saidizi vinapelekwa katika halmashauri 65 zenye vitengo na shule za mahitaji maalum ambazo hazikupata vifaa hivyo katika ugawaji wa awamu ya kwanza.

Alibainisha ugawaji wa vifaa hivyo ni moja ya malengo ya serikali ya kuwa idadi ya kutosha ya wananchi walioelimika katika sayansi na teknolojia na hivyo kukidhi mahitaji ya maendeleo ya taifa.

# TMA yawapa somo wakulima

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imewataka wananchi kutumia taarifa za mabadiliko ya hali ya hewa hususani kwenye shughuli za kilimo ili kujiepusha na hasara kwenye mazao wanayolima.

Akizungumza katika warsha iliyondaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Mkurugenzi wa Utafiti na Matumizi ya Hali ya Hewa wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema wananchi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kusikiliza taarifa za TMA ambazo zitawapa mwongozo wa kuendesha kilimo bila ya kupata hasara yoyote.

"Tunaomba mjenge utaratibu wa kutumia taarifa za TMA kwa sababu zitawasaidia kuepuka hasara mbalimbali zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa," alisema Dk. Chang'a.

Alisema mabadiliko ya hali ya hewa husababisha masuala ya ukame katika maeneo tofauti, hivyo kama watatumia taarifa za TMA, zitawasaidia pia kufanya utafiti sahihi na kutoa taarifa ya eneo husika linapaswa kulima mazao gani ili yastawi.

"Watafiti na viongozi wasisitiezeni wananchi kutumia taarifa za hali ya hewa,itasaidia kuepukana na changamoto za hasara ambazo zinajitokeza," alisema.

Kuhusu ujenzi wa madaraja, alisema wanapaswa wakandarasi kuzingatia taarifa za hali ya hewa ili kuepuka kutokea kwa maafa pindi wanapoendelea na ujenzi.

Naye, Dk. Goodluck Massawe, Mhadhiri wa Sera Mipango na Menejimenti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alisema ni vyema kuzingatia utafiti kuzingatiwa ili kufanya vitu kwa usahihi kulingana na matokeo chanya ya utafiti.

Hata hivyo, aliwataka wanasiasa kujenga utaratibu wa kutumia matokeo ya watafiti ili kuzungumza na wananchi wanaowaongoza katika masuala ya kilimo.

"Nawaomba wanasiasa mjenge utaratibu wa kufuatilia tafiti (utafiti) zinazofanywa (unaofanywa) na watafiti hususani katika suala la kilimo ili kuzungumza na wananchi wao," alisema.

# Waonywa kuwaficha watu wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

JAMII imeonywa kuwaficha watu wenye ulemavu katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti, mwakani, ili kupata takwimu sahihi zitakazotumika na serikali kutekeleza mahitaji yao kwa ufanisi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia, Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha wataalamu kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu kwenye sensa hiyo.

Alisema kutokuwepo kwa takwimu sahihi za watu wenye ulemavu imekuwa ni sababu kubwa kwa serikali kushidwa kutimiza mahitaji ya kundi hilo.

Pia alisema kuwa kitendo cha jamii kuwaficha watu wenye ulemavu wakati wa sensa wanaikosesha serikali kupata takwimu sahihi ambazo zingetumika kuwasaidia katika kero mbalimbali zinazowakabili.

"Maelekezo ya Rais wetu Samia (Suluhu Hassan) ni kwamba watu wenye ulemavu bado wana shida nyingi lakini hili sababu kubwa ni kukosekana kwa takwimu sahihi, hivyo tushirikiane katika sensa ya 2022.

"Pia kupata takwimu sahihi za idadi ya walemavu katika maeneo yote na aina ya ulemavu wao ili kuweza kuzishughulikia ipasavyo changamoto zao," alisema.

Aidha, alisema kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika sensa hiyo imetenga bajeti ambayo itatoa suluhu ya upatikanaji wa takwimu sahihi ya idadi ya watu wenye ulemavu nchini.

Kadhalika, alisema kama ambavyo Umoja wa Mataifa unaagiza kuwa hakuna kumwacha mtu nyuma ni jukumu la taifa kuhakikisha kila kundi linahusishwa katika jambo hilo.

"Pamoja na maagizo hayo lakini pia sisi kama taifa tumeridhia mikata mbalimbali ya kulinda haki za watu wenye ulemavu lakini pia zipo sera pamoja na sheria za nchi ambazo tunatakiwa kuzilinda," alisema.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema katika sensa hiyo wamejipanga kuhakikisha kila kundi linajumuishwa ili kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kulisaidia taifa kutekeleza majukumu yake.

"kazi iliyoko mbele yetu ni la kitaifa na linashirikisha makundi yote. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) tutahakikisha makundi yote katika jamii yanashirikishwa ili kupata takwimu sahihi," alisema Dk. Chuwa.

Vile vile, alisema takwimu zinaonyesha kuwa kundi la watu wenye ulemavu ni kubwa hasa kwa nchi zinaendelea na hasa katika bara la Afrika. "Kwa bara la Afrika idadi ya watu wenye ulemavu ni asilimia 40, hivyo suala la watu wenye ulemavu si jambo la mzaha, tunahitaji mipango imara," alisema.

# Wanawake wachagizwa kujiendeleza kibiashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amewataka wanawake kujiendeleza kibiashara na kuacha utegemezi ili kujikwamua kiuchumi.

Akifungua kongamano la tatu la Ustaarabu wa Mwanamke katika Ukumbi wa Sanaa Raha Leo, Zanzibar, alisema wanawake ndio dira ya maendeleo katika jamii, hivyo yuko tayari kutoa ushirikiano ili kuleta maendeleo kwa wanawake.

Alisema Ustaarabu wa Mwanamke unajegwa na heshima, uzalendo pamoja na uaminifu, hivyo lazima wapambane ili kufikia malengo yao.

Zainab alisema Wazanzibari wana ustaarabu wao katika malezi kwa kuwa wana wajibu wa kuutumia ustaarabu huo kwa lengo la kupata malezi bora kwa vizazi vijavyo.

Pia aliwataka wanawake wa Zanzibar kuachana na mambo yasiyo na faida katika maisha yao na kujikita zaidi katika shughuli ambazo zitaleta tija na maendeleo katika jamii ikiwamo ujasiriamali.

Akitoa maana ya Ustaarabu wa Mwanamke, Mwanaharakati wa Masuala ya Kijamii, Raya Hamad, alisema mwanamke awe na uwezo wa kufikiri kitu ambacho kina manufaa kwa jamii na baadhi yao hawafahamu majukumu yao.

Kwa upande wao, wanafunzi waliopatiwa mafunzo katika kongamano hilo, walisema kuwa wamejifunza kuondokana na utegemezi kwa kufanya kazi mbalimbali za kujiendeleza kiuchumi ikiwamo kutengeneza mikoba.

"Kiukweli tumejifunza mambo mengi sana ambayo tulikua hatuyajui na yanaweza kutupatia fursa za maendeleo na kujiendeleza kwa kupanua biashara zetu," alisema Asha Juma, mwanafunzi wa Chuo cha Habari Zanzibar.

Aliwashauri vijana kuacha kutegemea ajira kutoka serikalini na kuacha woga jambo ambalo hurudisha nyuma jitihada za kujikwamua kiuchumi.

Kongamano hilo la siku nne ambalo mada mbili zimejadiliwa zikiwamo kujitambua na afya ya jamii, lina kauli mbiu isemayo: "Mwanamke Kamata Fursa Dunia Inakusubiri."

# Sababu kuchelewa ujenzi hoteli zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Pannyroyal Limited imesema mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.6 umechelewa kuanza kwa kasi kutokana na uhaba wa mchanga na maradhi ya corona yaliojitokeza duniani.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Saleh Mohamed Said, alisema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja wakiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo wakisimamia Ilani ya Uchaguzi mwaka 2020 - 25.

"Kuna sababu nyingi zimefanya kuchelewa awamu ya kwanza ya ujenzi wa hoteli ya nyota tano ikiwamo kuchelewa kupatikana kibali cha ardhi, uhaba wa mchanga na maradhi ya corona yaliyojitokeza duniani na kuathiri sekta ya uchukuzi na usafirishaji," alisema Saleh.

Alisema mradi ulianza mwaka 2015 kwa hatua za kusajiliwa Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) lakini kibali cha ardhi kilichelewa kutokana na kupatikana mwaka 2018 kikiwa na makosa na kulazimika kufanyiwa marekebisho.

"Kuchelewa kwa barabara inayoelekea katika mradi pia kulizorotesha utekelezaji na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi kutoka nje ya nchi. Lakini sasa makotena yetu yakiwa na vifaa vya ujenzi yamewasili Zanzibar," alisema.

Saleh alisema mradi huo unatarajia kugharimu dola za marekani Bilioni 1.6 na tangu kuanza kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji, Dola milioni 40 zimetumika mpaka mwaka huu.

Saleh alisema vijana 700 watanufaika na ajira baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi mwakani na mradi huo utasaidia kuitangaza Zanzibar pamoja na kusadia serikali katika utekelezaji wa mpango wa uchumi wa buluu.

Pia alisema kampuni imekuwa ikisaidia huduma za jamii katika sekta za elimu, uhifadhi wa mazingira na watu wenye mahitaji maalum katika vijiji vya Mtemwe Mbuyutende na kijini Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Meneja wa Mradi, Murtaza Hassanal, alisema wanakabiliwa na uhaba wa mchanga, hivyo kusababisha kasi ya ujenzi kupungua.

"Mahitaji yetu ya mchanga awamu ya kwanza ya ujenzi ni tani 15,000 lakini mpaka sasa tumetumia tani 4,000. Tukiomba kibali cha mchanga tunapatiwa tani 300 au 400. Kwa kweli mchanga ni changamoto kubwa katika mradi huoo," alisema Murtaza.

Alisema waliomba serikali kuwapatia eneo la kuchimba mchanga na baada ya ujenzi kukamilika sehemu ya shimo uanzishwe mradi wa kufunga samaki na uhifadhi wa miti na kuwasadia wanakijiji lakini maombi hayo yamekwama mpaka sasa.

Pia alisema hoteli hiyo itakuwa na michezo ya baharini, uwanja wa mchezo wa gofu, na kila nyumba itakuwa na bwawa la kuogelea pamoja na sehemu za burudani.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, aliwataka vijana kutumia fursa za ajira zinazoendelea kujitokeza kupitia ujenzi wa hoteli za kitalii badala ya kuchagua kazi na kulazimika kampuni za ujenzi kuajiri watu kutoka nje ya Zanzibar.

Alisema mraidi huo wa ujenzi wa hoteli hiyo, utasadia kuongeza ajira kwa vijana, wavuvi, wakulima na wajasiriamali na kuwataka wavuvi kuingia katika uvuvi wa bahari kuu ili kutumia soko la sekta ya utalii Zanzibar.



Mkurugenzi wa kampuni ya Pannyroyal Ltd, Saleh Said Muhammed (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu kuchelewa kwa mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano huko Matemwe Mbuyu Tende, Mkoa wa Kaskazini Unguja kutokana na uhaba wa mchanga na maradhi ya corona yaliojitokeza duniani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaahidi Kenya ushirikiano zaidi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendeleza ushirikiano wake na Kenya kupitia sekta mbalimbali ikiwamo uwekezaji.

Hemed alisema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wanaowakilisha wananchi kutoka Bunge la Kenya walipofika ofisini kwake, Vuga.

Alisema serikali imefungua milango kwa kuwakaribisha wawekezaji Zanzibar kuwekeza, hivyo akawataka viongozi hao kuitumia fursa hiyo kwa kuwaeleza wananchi wa Kenya juu ya fursa zinazopatika.

Hemed alisema viongozi wakuu wa nchi za Tanzania na Kenya tayari wameshaonyesha nia njema ya ushirikiano mwema kwa raia wake huku akisisitiza hakutakuwa na vikwazo vyovyote kwa watakaotaka kuwekeza Zanzibar.

Kwa mujibu wa Hemed, hivi sasa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetilia mkazo katika uwekezaji kwa kukuza uchumi wake na kwamba Rais wa Zanzibar ameanzisha Wizara maalum inayohusiana na uchumi wa buluu.

Naye Kiongozi Msaidizi wa Msafara wa Wabunge, Musili Mawathe alisema faraja waliyo nayo juu ya hatua ambazo Zanzibar inaendelea kuzichukua katika kupambana na corona.

Akiwasilisha salamu za Spika wa Bunge la Kenya, kiongozi huyo aliahidi kwamba serikali ya Kenya itaendeleza ushirikiano uliopo kati ya Kenya na Tanzania kupitia sekta ya mbalimbali ikiwamo biashara.



**ALI KIBA TENA NA TENA ...'SALUTE'** Uk.14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JUNI 26, 2021



# Kwani wenyewe wanasemaje?

MWANAMUZIKI nyota nchini, Diamond Platnumz, na mzazi mwenzake Zari, wanatabiriwa kuwa kivutio katika kipindi kipya cha televisheni kinachohusu maisha halisi ya kiafrika.

Kipindi hicho ambacho kitawakutanisha mastaa kutoka nchi mbalimbali za kiafrika, kitaendeshwa na mtangazaji maarufu wa Ghana, Peace Hyde, na kuonekana katika mtandao maarufu wa Netflix.

Wiki hii, mtangazaji huyo ambaye ana uraia wa Uingereza, aliandika katika ukurasa wake wa Instagram, akitaka mashabiki wake kusubiri kazi mpya ambayo itaonyesha maisha halisi ya Kiafrika kutoka kwa wasanii hao.

"Tunafanya jambo la historia ya Kiafrika kwa kusimulia hadithi zetu na nimeheshimu sana, nimefurahi na niko tayari."

Kipindi hicho kitawakutanisha Diamond Platnumz kutoka Tanzania, Annie Idibia, Swanky Jerry kutoka Nigeria, Zarina Hassan " The Boss Lady " kutoka Uganda, na wasanii maarufu wa Afrika Kusini, Nadia Nakai, Khanyi Mbau, Andile Ncube na Naked DJ.

Hata hivyo, macho ya mashabiki yatakuwa kwa Diamond na Zari kutokana na mvuto wa maisha na jinsi wanavyoweza kugeuza upepo kila mara na watu wakawafuata.

BASI SAWA

## Chege moyo wake unalia, usoni bashasha tele



MWIMBAJI kutoka Temeke, Chege, amesema ametokea katika familia masikini na kila anapokumbuka aliyoyapitia anakuwa na uchungu, japokuwa usoni anaonekana ana furaha.

Amesema kutokana na maisha yake, amefanya mambo mengi kama kurudisha upendo wake kwa jamii, lakini kutokana na imani yake hawezi kuyaweka wazi.

"Kutokana na imani yangu unaposaidia inakuwa siri yako na Mungu, hivyo siwezi kusema hadharani nini nimefanya. Tunatakiwa tuishi kama kioo cha jamii, mienendo yetu inafuatiliwa kila siku," amesema.

## Ali Kiba tena na tena ...'Salute'



MSANII Nyota wa Bongo Fleva na kiongozi wa lebo ya Kings music, Alikiba, hatimaye ameachia ngoma yake mpya akimshirikisha mwanamuziki wa Nigeria Rudy boy.

Wimbo huo ambao unaitwa 'Salute' aliutambulisha rasmi wiki hii.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Ali kiba ameandika "Mashabiki wangu natimiza ahadi kwenu, narudia tena kuse- ma ni mwendo bandi- ka bandua,"ameandika kwa lugha ya kingereza.



## Shilole wapashe wasanii

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya na mjasiriamali, Shilole, amesema kama wasanii wa muziki watajiheshimu na kuwa na maadili mema, wataonekana na kuteuliwa katika ngazi mbalimbali za serikali.

Shilole, amesema rapa Niki wa Pili ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, uteuzi wake unatokana na kuwa mtu wenye sifa zote na sio upendeleo.

"Nawasihi wasanii wezangu kama wakiendelea kuwa na tabia ya kutojiheshimu, kupenda kiki chafu basi uteuzi wa serikali watausikia katika bomba tu, mama Samia anaangalia maadili ya mtu," amesema Shilole.





## Erica Lulakwa atoa siri ya 'Chereko'

MSANII wa kikazi kipya anayeishi Marekani, Erica Lulakwa, maarufu kama Twiga, amesema ataendelea kutumia lugha ya Kiswahili ili kuitangaza na wimbo wake mpya ameupa jina la Chereko.

Akizungumza na BT, Erica amesema ngoma hiyo yenye mahadhi charanga na mduara imepokewa vizuri na anaamini yeyote atakayesikiliza hata kama hajui Kiswahili ataupenda.

"Naendelea kutumia Kiswahili katika nyimbo zangu sababu ndo lugha mama pili napenda muziki wangu ueleweke kwa Watanzania pia hii ni njia moja wapo ya kuitangaza lugha ya Kiswahili,".

Ameongeza "Mpaka sasa Chereko imepokelewa vizuri sana na mtu yeyote akiisikia anaipenda ghafla, inapatikana majukwaa yote ya kidijitali ya kuuza na kusikiliza muziki,"

## Hata mikoani kulitisha

**Na Adam Fungamwango**

KUNA uhaba mkubwa wa bendi za muziki wa dansi kwa sasa.

Si mikoani tu, bali hata jiji la Dar es Salaam ambalo lilijulikana kwa chimbuko la bendi nyingi za dasi, nalo linakabiliwa na uhaba.

Hapa nataka nikutajie tu jinsi gani alivyozitaja kwa kuimba. Lengo ni kukuonyesha ni jinsi gani bendi zilivyokuwa nyingi. Na alizozitaja karibuni zote ni za Dar es Salaam.

"Ukiwakosa wana Kamanyoka kupitia Sikinde Ngoma ya Ukae. Usisahau Msondo Ngoma, Wana Chakachua pia usubiri. Mwendo wa Jongoo na Super Bomboka huporomosha. Mwenge ya Mashujaa, Kimulimuli huporomosha. Mzee Makassy, Polisi, Kumbakisa huporomosha, Wana Kimbunga na UDA pia huporomosha." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo wa Kikumbi Mwanza Mpango, aliyeimba mwaka 1980.

Hii inaonyesha kuwa zamani kulikuwa na bendi nyingi sana. Na zote zilikuwa zinapiga muziki mzuri na kuwa na wanamuziki maarufu sana nchini. Leo tutaziangalia baadhi ya bendi zilizokuwa za mikoani na ambazo zilikuwa tishio kwa bendi kubwa za Dar es Salaam.

**MOROGORO JAZZ BAND**

Ni moja kati ya bendi maarufu sana nchini Tanzania, Afrika Mashariki na tishio kwa bendi za jijini Dar es Salaam kama Dar Jazz, Western Jazz, Nuta Jazz, na nyinginezo.

Ikumbukwe kuwa bendi hii ndiyo alikuwa akiipigia Mbaraka Mwinshehe. Kwa maana hiyo haihitaji maelezo mengi sana kujua umahiri wake. Cha kuongeza ni kwamba mkoani Morogoro kulikuwa pia na bendi nyingi kali kama Cuban Marimba, Kilombero Jazz, Kilosa Jazz, Ulanga Jazz na nyinginezo.

**JAMHURI JAZZ BAND**

Hii pia ni moja kati ya bendi zilizotingisha nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Maskani yake ilikuwa ni Tanga. Hii ndiyo bendi ambayo wametokea wanamuziki waliokwenda kuunda bendi ya Simba Wanyika na kutia fora nchini Kenya, Wilson Peter na mdogo wake, George Peter.

Mbali na bendi hiyo, Tanga kulikuwa na bendi nyingine kali, Atomic Jazz na Amboni Jazz ambazo pia zilifanya vema sana.

**KURUGENZI JAZZ BAND**

Mkoani Arusha kulikuwa na bendi iliyoitwa Kurugenzi Jazz. Ni bendi ambayo nayo ilikuja kutetemesha bendi nyingi nchini. Nyimbo kama 'Wivu' na 'Ujamaa Hautakufa', zilipigwa na bendi hii.

Asili ya bendi hii ni wanamuziki wa Morogoro waliojiengua kutoka Morogoro Jazz, Cuban Marimba, na Super Volcano waliokuwa nchini Kenya na kuunda bendi ijulikanayo Orchestra Lombe Lombe.

Baada ya kupokonywa vyombo nchini Kenya kwa kukiuka masharti ya mikataba, Halmashauri ya Arusha iliwapa vyombo na kuwahamisha kutoka nchini humo na kuleta hapo na kuwa Kurugenzi Jazz. Hata wimbo wa 'Wivu' upo ambao ulirekodiwa Kenya, wakati huo ikiwa Lombe Lombe.

**TABORA JAZZ BAND**

Bila shaka haihitaji maelezo mengi kujua kuwa hii ni bendi maarufu, kubwa na bora kabisa nchini Tanzania ikiwa na maskani yake mjini Tabora.

Mbali na Kutamba na vibao kama 'Dada Asha', imetoa wanamuziki bora waliokwenda kwenye bendi nyingi kama Shem Karenga aliyekwenda KM Beats 'Tukunyema', Msafiri Haroub aliyekwenda Mwenge jazz.

**TANCUT ALMASI ORCHESTRA**

Ni bendi ya mkoani iliyokuwa na wanamuziki wa Kikongomani wengi kuliko nyingine yoyote ile nchini. Kyanga Songa, Kasaloo Kyanga, Kawele Mutinamwa, Kalala Mbwebwe, Kabaa Belela na wengineo. Ilitamba kwenye miaka ya 1980. Ilikuwa ikija Dar, bendi zote zinakimbia mji na kukimbilia kufanya ziara mikoani kuwakimbia. Makao yao yalikuwa ni Iringa. Walijiita Mabush Stars 'Kinye kinye kisonzo tisa kumi Mangala'.






## Deception; Mapenzi dawa, pia ni sumu kali

**Na Adam Fungamwango**

WAKATIi mwingine binadamu unaweza kupata matatizo makubwa. Au watu unaowaamini wanaweza kukufanyia mambo ambayo hukutarajia kuwa wanaweza kukufanyia.

Mara nyingi hapo mtu hujawa na hasira na kuweza kufanya jambo lolote lile baya, ili mradi tu kuonyesha kuchukizwa na kile ulichofanyiwa.

Hili limeonekana kwenye filamu ya 'Deception'. Imechezwa na Kanumba mwenyewe, aliyekuwa rafiki yake mkubwa Patcho Mwamba, Rose Ndauka, Sethi Bosco na wengineo.

Patcho na mkewe Rose wanaishi maisha mazuri, wakiwa na kila kitu ambacho kinahitajiwa ili ndoa yao iwe na furaha na amani.

Hata hivyo mwanamama huyo anaingia kwenye penzi na jamaa mmoja wa mtaani ambaye hata pesa zake za kutanua tu, anazipata kwa kumuomba mama yake.

Huyu si mwingine bali na Kanumba. Anaiingilia ndoa ya Patcho, kiasi mpaka mwenyewe anahisi kuwa kuna kitu ambacho si cha kawaida.

Kuna siku Rose anapigiwa simu kutoka Songea kuwa mama yake ni mgonjwa sana.

Haikuwa hivyo, Simu ile ilikuwa ni magumashi matupu. Ilitengezwa tu ili aende kutanua na mpenzi wake Kanumba.

Pamoja na Patcho kumsindikiza mkewe hadi kwenye kituo cha mabasi Ubungo na kuhakikisha mpaka basi linaondoka, Rose anashukia njiani na kwenda moja kwa moja hadi kwa mpenzi wake Kanumba. Wanakwenda kwenye hoteli moja maarufu hapa jijini kwenda kustarehe, hadi siku alizopewa mwanamama huyo na mumewe kuuguza mgonjwa zimalizike.

Asubuhi wakati Kanumba anakwenda kuagiza supu kwa ajili ya mpenzi wake, aliporejea anamkuta amekuwa maiti. Anachanganyikiwa hajui nini kimetokea. Anatoroka, lakini anaangusha kitambulisho.

Mlinzi Seth, anamnong'oneza mmoja wa wahudumu kuwa mteja wao hakufa kifo cha kawaida, bali aliuawa na muuaji aliwahi kumuona.

Siku mbili baadaye naye anauawa akiwa hospitalini alipokuwa amelazwa. Lakini muuaji anasahau simu. Polisi wanataarifiwa muuaji wa mgonjwa hospitalini amesahau simu, lakini wanapofika daktari anawaambia kuwa walivamiwa na mtu mmoja mwenye silaha ambaye aliwanyang'anya simu.

Mauaji hayo yanawaumiza kichwa polisi. Hata hivyo kuna mtu mmoja anajitokeza polisi na kusema kuwa ana mkanda wote wa mauaji hayo.

Anawaambia kuwa yeye mwenyewe amelishwa sumu, hivyo wakati wowote anaweza kufa, lakini kabla hajafa, ayaanike yote.



# Teni avunjika mkono akirekodi video

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Teni, amevunjika mkono wake wa kulia wakati akitayarisha video ya wimbo mpya kutoka kwenye album yake 'Wondaland' aliyoiachia hivi karibuni.

Staa huyo ambaye ni bilionea ameweka picha zake katika mtandao wa kijamii zikionyesha matukio mbalimbali wakati akitayarisha video hiyo ambapo ameonekana akiwa kwenye kiti cha mbele cha gari lililokuwa limening'inizwa hewani huku yeye akiimba wimbo huo.

Album ya 'Wondaland' ina nyimbo 17 ambazo zimeleta hisia kwa mashabiki wake.



## R Kelly apelekwa gereza lingine

MWANAMUZIKI wa R&B, R. Kelly, amehamishiwa gereza lililopo mjini Brooklyn, New York nchini Marekani akisubiri kesi yake kuanza kusikilizwa mwezi Agosti mwaka huu.

Tovuti ya magereza hiyo, imethibitisha kuwa siku ya Jumatano wiki hii, Kelly aliwasili katika Gereza la Metropolitan Detention Center huko Brooklyn.


Tangu mwaka 2019, R. Kelly alikuwa akishikiliwa katika Gereza la MCC kwa makosa matatu ya unyanyasaji wa kingono kwa wasichana wenye umri mdogo.

## Chris Brown ungejiunga ngumi

RAPA mkali wa Marekani, Chris Brown, anachunguzwa kwa kumshambulia mwanamke nyumbani kwake.

Kulingana na mtandao wa TMZ, msanii huyo alimpiga kichwa mwanamke huyo ambaye hajatambuliwa eneo la kisogoni na kusababisha wigi alilovaa kuvuka.

Katika tukio hilo hakuna mtu aliyekamatwa, lakini polisi wanachunguza tukio hilo pamoja na eneo la nyumba hiyo iliyotumiwa kufanya shambulio hilo.





## Duh! Shola miezi 5 hukula mbilimbi

SHOLA Ogudu, ambaye ni mama wa mtoto wa kwanza wa mwanamuziki kutoka Nigeria, Wizkid, amesema ujauzito wake wa kwanza hakuweza kujua hadi ulipofikia umri wa miezi mitano.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, mwanamama huyo alichangia swali kwamba inakuwaje mwanamke kutofahamu hali yako ya ujauzito ndani ya miezi mitatu? Shola alijibu jambo hilo linawezekana..

"Inawezekana kabisa, nasema haya kutokana na uzoefu wangu, kwani baada ya kubeba ujauzito wangu wa kwanza sikujua na niliendelea kuona hedhi kwa muda wa miezi mitano," amesema Shola

## Eacharia msamehe tu, hakuna kama baba

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Eucharia Anunobi, amesimulia jinsi baba yake alipokataa kumpeleka shule, kisa yeye ni mwanamke.

Kulingana na posi aliyoiweka katika akaunti yake ya Instagram,nyota huyo wa filamu ameyasema hayo wakati akikumbuka malezi mabaya kutoka kwa baba yake.

"Angalia ikiwa wewe ni msichana ambaye baba yako tajiri alikataa kukupeleka shule ya upili, labda inatokana na kutokuwa na hitaji la mtoto wa kike. Kwamba jinsia ya kike haina maana kwake na haiwezi kubeba jina lake popote. Kiujumla yeye aliwaelimisha watoto wa kiume kwa kiwango chochote cha elimu," amesema Eucharia.



MAKALA

# Ndivyo ujasiriamali TASAF unavyowanusuru maskini

**Na Marco Maduhu, SIMIYU**


Wanakikundi cha wanawake katika Kijiji cha Ngulyati walianzisha kikundi cha ujasiriamali kujikwamua na umaskini. **PICHA: MARCO MADUHU**

MPANGO wa kunusuru kaya maskini unaofanywa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), licha ya kuziinua kaya maskini kiuchumi, waratibu wa mfuko huo kwa kila halmashauri pamoja na kuwapa rasilimali za kujikimu, huwafunza wanufaika mbinu za ujasiriamali ili kuongeza kipato na kuondokana na umaskini.

Hayo hufanyika sambamba na kutoa fedha za ruzuku kwa walengwa hao, wanaopatiwa elimu ya kutumia ruzuku na ya ujasiriamali, ili fedha hizo wazitumie vizuri na kuwaondoa kwenye ufukara na maisha duni.

Mratibu wa TASAF katika Halmashauri ya Bariadi mkoani Simiyu, Caphline Budodi, anasema waliamua kuwapatia elimu hiyo ya ujasiriamali walengwa wote wilayani humo, wakiamini ndiyo njia sahihi ambayo itawainua kiuchumi na kuaga umaskini.

Anasema awali walengwa wa TASAF wilayani humo, walikuwa wakizitumia fedha hizo ovyo kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya ujasiriamali, namna ya kuzitumia vizuri na kujikwamua kiuchumi,

Aidha, anasema baada ya kugundua kuwapo na changamoto hiyo, ndipo wakaanzisha mkakati wa utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa walengwa hao ili fedha hizo za ruzuku wazitumie kuwekeza kwenye shughuli za uzalishaji na kupata kipato ambacho kitawainua kiuchumi na kuondoka kuishi maisha ya umaskini.

"Elimu hii ya ujasiriamali imekuwa na mafanikio makubwa kwa walengwa wa TASAF kujikwamua kiuchumi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi wengi wamejenga nyumba, wana mifugo na kulima kupitia shughuli zao za ujasiriamali," anasema Budodi.

"Tangu mpango huu wa kunusuru kaya maskini uanze katika halmashauri yetu hii ya Bariadi mwaka 2015, mpaka sasa tumeshatoa kiasi cha fedha Sh. bilioni 11.6 kwa walengwa 5,870 na tumekuwa tukiwatembelea mara kwa mara ili kuona maendeleo yao ya kujikwamua kiuchumi," anaongeza Budodi.

Baadhi ya walengwa wa TASAF ambao wamejikwamua kiuchumi kupitia shughuli za ujasiriamali ambao wanaishi katika Kijiji cha Ngulyatia Bariadi mkoani Simiyu, wanasimulia namna fedha hizo zilivyowakwamua kimaisha.

Helena Amos ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Wanawake Tushirikiane cha kijijini humo, anasema awali kabla ya kuingia kwenye mpango huo, alikuwa na maisha magumu, lakini kwa sasa mfumo wake wa maisha umebadilika na siyo maskini tena.

Anasema mwaka 2015 alipokuwa akipata Shilingi 32,000 alianza kufanya shughuli za mamalishe ya kuuza chakula kijijini humo na baada ya kupata faida alianza kujenga nyumba, na sasa anaishi kwenye nyumba ya bati, huku pia akisomesha watoto wake shule na kukidhi mahitaji yake mengine ya nyumbani. Anasema mwaka 2018, aliwaita wenzeka watatu ambao ni walengwa wa TASAF kijijini humo na kisha kuzungumza nao namna ya kuunganisha nguvu ya pamoja kwa kuchangishana fedha, ili wakuze mtaji na kuanzisha utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za kiujasiriamali ambazo zitawapatia kipato kingi.

Anasimulia kuwa baada ya hapo wakachangishana fedha akatumia elimu yake kutengeneza sabuni za maji kwa ajili ya usafi, mafuta ya kupaka, sabuni za maji za kuoshea nywele na kutengeneza vitenge vya batiki na aliwafundisha wenzake hao ndipo wakaunda kikundi chao, ambapo walengwa wengine waliongezeka na kufika watu nane hadi sasa.

Anasema baada ya hapo walianza shughuli hiyo ya utengenezaji wa bidhaa na kuanza kuuza kijijini humo, ambapo soko lake lilikuwa kubwa kutokana na uhitaji wa watu ikiwamo na kwenye huduma za kiafya na shuleni, na hatimaye kuongeza wigo wa shughuli yao na sasa hawaishi tena maisha magumu kama zamani.

"Kila mmoja unayemuona hapa kwenye kikundi chetu siyo maskini tena, baadhi wamejenga nyumba za bati, wana viwanja, mashamba, wana mifugo, wanasomesha watoto chuo, kupitia utengenezaji huu wa bidhaa zetu za ujasiriamali," anasema Amosi.

Katibu wa kikundi hicho Marysiana Ladslaus, anasema alikuwa hana ujuzi wowote, lakini baada ya kupata elimu ya ujasiriamali imempatia maarifa namna ya kutafuta fedha za kumtoa kwenye umaskini.

Anasema kwenye kikundi chao hicho cha ujasiriamali kila baada ya miezi sita wanagawana faida, fedha ambazo kila mmoja ameanzisha shughuli yake nyingine ya biashara, ambayo inamwingizia kipato cha ziada, tofauti na fedha za kikundi, pamoja na kukidhi mahitaji ya nyumbani.

"Elimu hii ya ujasiriamali imekuwa mkombozi mkubwa sana kwangu kunitoa kwenye maisha ya umaskini, sasa hivi nimenunua cherehani nashona nguo na kupata fedha, nina mbuzi wanne, nyumba zangu mbili nimeezeka bati na kutoa majani, fedha ambazo zimetokana na utengenezaji huu wa sabuni, mafuta ya kupaka na batiki," anasema Marysiana.

Christina Ngenzi ni miongoni mwa wanakikundi cha ujasiriamali cha walengwa wa TASAF kijijini Ngulyati, anasema mbali na kufanya shughuli hizo za kikundi, pia anajishughulisha na biashara za genge la mboga zikiwamo nyanya na kujipatia kipato cha ziada.

Anasema faida ambayo ameipata hadi sasa amefanikiwa kununua viwanja viwili kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ana mabati 10 ndani, na pia anasomesha watoto wake kwa kuwatimizia mahitaji yote ya shule, na kuishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo wa TASAF ambao umekuwa mkombozi kwa wanyonge.

Mtendaji wa kijiji hicho cha Ngulyati Godwini Misana, ambaye ni mlezi wa kikundi cha ujasiriamali cha walengwa wa TASAF, anasema baada ya walengwa hao kuanza kujihusisha na ujasiriamali hali ya kiuchumi ya kaya hizo imeimarika tofauti na hapo awali, ambapo walikuwa wakiulizia fedha zinakuja lini sababu ya fedha kuisha na kuendelea kuishi maisha magumu.

Anasema baada ya kuanza shughuli hiyo ya ujasiriamali na utengenezaji wa bidhaa za sabuni za usafi, mafuta ya kupaka, shampoo na batiki, huku pia wakiendelea kila moja na biashara zake, kwa sasa hawasumbui tena kama zamani ikiwa vipato vyao vimeongezeka na wanakidhi mahitaji ya nyumbani kwao.

Aidha, anasema ameshakisajili kikundi kwenye halmashauri kwa ajili ya kupata mkopo wa wanawake, vijana na wenye ulemavu, fedha ambazo zitawasaidia kupanua soko la bidhaa zao na hata kuanza kuuza kwenye mikoa mbalimbali.

"Kijiji changu cha Ngulyati nina walengwa wa TASAF 241, na mpaka sasa kiasi cha Sh. 9,560,000 kimeshatolewa kwa ajili ya kuzinusuru kaya maskini na kuwainua kiuchumi," anasema Misana.

Pia anasema wamekuwa wakiwatembelea walengwa kijijini humo mara kwa mara, na kuwashauri matumizi sahihi ya fedha hizo kuwakwamua kiuchumi, ambapo baadhi yao wamejikita kwenye ufugaji na kilimo.

MAKALA

# CRB na mkakati kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo

**Na Joseph Mwendapole**

MIRADI mingi ya ujenzi yenye gharama kubwa inafanywa na kampuni za kigeni, hali ambayo serikali inasema haipendezi kutokana na fedha nyingi zinakwenda nje ya nchi.

Serikali mara kadhaa imesema ingependa kuona kazi hizo za miradi yenye gharama kubwa zinafanywa na kampuni za wazalendo ili fedha nyingi zibaki hapa nchini na kusisimua uchumi wa nchi kwa kujenga miradi mingine.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), inasema ingawa miradi mingi ya ujenzi inafanywa na makandarasi wazalendo karibu asimilia 96, lakini fedha kwenye miradi hiyo ni ndogo sana kulinganisha na asilimia 3.1 ya miradi inayofanywa na kampuni za kigeni.

Ili kugeuza hali hiyo CRB, sasa imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo kuhakikisha wanakuwa na uwezo wa kushindana na makandarasi kutoka nje.

Katika jitihada hizo kwa mwaka huu pekee CRB imefanya mikutano minne ya kikanda ili kuwafikia makandarasi wengi nchini.

Mikoa iliyohusishwa ni Mbeya, Arusha, Dar es Salaam na Mwanza ambapo mamia ya makandarasi wamekuwa wakibadilishana uzoefu.

Kwenye mikutano hiyo makandarasi wamekuwa wakikutanishwa na wateja mbalimbali wakopeshaji kutoka benki mbalimbali, watunga sera na wateja hivyo kujadiliana kwa kina kuhusu sekta hiyo.

Miongoni mwa juhudi zilizofanywa na CRB, ni kuanzisha mfuko wa kuwakopesha makandarasi wanapopata kazi za ujenzi ujulikanao kama Contractors Assistance Fund (CAF).

Mfuko huo umekuwa mkombozi kwa makandarasi wengi kwani bila kujali madaraja waliyonayo, wanaweza kukopa na kuendelea na miradi ya ujenzi na kurejesha baada ya kukamilisha miradi yao.

Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori, anasema mfuko huo umekuwa msaada mkubwa kwa makandarasi kudhaminiwa kukopa benki ya CRBB kupata dhamana kwa ajili ya zabuni na malipo ya awali yaani 'advance payment Guarantees'.

Msajili anasema mwaka 2020, CRB ilifanya majadiliano na benki ya CRDB na kufikia makubaliano ya kudhamini makandarasi wa ndani wa madaraja yote badala ya makandarasi wadogo na wakatikama ilivyokuwa awali na kuongeza kiwango cha dhamana kutoka Sh. milioni 50 hadi 100.

Serikali kwa upande wake imesema itaendelea kutenga miradi maalum kwa ajili ya kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, anasema serikali inatamani sana makandarasi wazalendo wawe na uwezo wa kushindana na makandarasi wa nje kwenye miradi mikubwa kwani kutasaidia gharama za miradi hiyo kupungua.



Daraja la mawe linalojengwa na makandarasi wa ndani mkoani Kigoma.

Anasema ni dhahiri kwamba iwapo kazi hizo kubwa kubwa za miradi ya ujenzi zitafanywa na kampuni za makandarasi wazalendo fedha nyingi sana zitabaki nchini na kufanya shughuli zingine za ujenzi wa miradi.

Ili waweze kufanikiwa kwa urahisi Waziri aliwaasa waache ubinafsi na kuungana ili wapate nguvu ya mitaji na ujuzi wa kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi yenye thamani kubwa.

Anasema serikali itafurahi kuona uwezo wa makandarasi wazalendo ukiimarika kwani wataweza kushindana na makandarasi wageni hivyo kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi na fedha nyingi kubaki nchini kufanya kazi zingine.

"Acheni ubinafsi mfanye kazi kwa ubia, mkiungana ndipo mtapata uwezo wa kimitambo na utaalamu wa kushindanaa na wenzetu wa nje kwa sababu hata hao wa nje mnaona wanafanyakazi kubwa kubwa hawako mmoja mmoja wengi ni kwasababu wameungana na kupata nguvu," alisema Waziri Chamuriho.

**KUHUSU 'FORCE ACCOUNT'**

Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Mhandisi Consolatha Ngimbwa, amekuwa akiiomba serikali mara kadhaa kuachana na utaratibu wa kufanyakazi yenyewe kwa utaratibu wa kutumia 'force account'.

Anasema serikali iliamua kufanya hivyo kwa maelezo kuwa baadhi ya makandarasi wazalendo walikuwa wakiweka bei za juu kwenye miradi yake lakini kwa sasa wameshabadilika na wako tayari kufanya kazi.

Alisema CRB iliamua kuanza kutoa mafunzo maalum kwa makandarasi kwa ajili ya kujaza zabuni tangu mwaka 2018 wamekuwa wakiwapa kozi hizo kwenye mikoa ya Morogoro, Arusha, Njombe, Dar es Salaam, Bukoba, Mwanza kwa ajili ya kuwatayarisha makandarasi waingie kwenye ushindani miradi ya serikali.

"Makandarasi walishiriki mafunzo kwa wingi na kwa uhakika wako tayari kufanya hizo kazi na mfano mzuri ni jengo letu la Dodoma wakati ule linawekewa jiwe la msingi, Rais wa awamu ya tano Hayati John Joseph Magufuli alifurahishwa na bei ambazo makandarasi wetu walitoa na alitaka tuendelee kutoa bei nafuu," alisema.

Mhandisi Ngimbwa naye mara kadhaa amekuwa akiwaambia makandarasi wazalendo waache ubinafsi waungane ili wapate nguvu za kushindana na wenzao wa makampuni ya nje kwenye kandarasi kubwa kubwa. Wakati alipofunga mkutano huo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliwataka makandarasi wanaofanya kazi kwa ubia wametakiwa kuacha tabia ya kugawana faida kabla ya miradi wanayoifanya kukamilika kwani hali hiyo husababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati.

Alisema makandarasi wengi wazalendo wamekuwa wakikwama kutokana na tamaa ya fedha mara wanapopata miradi tofauti na wenzao wa China ambao hugawana faida baada ya kumaliza kazi na wamekuwa wakijituma kutokana na kufuatiliwa na nchi yao.

"Nimetembea miradi mingi hapa nchini nimekuta mingi sana wanafanya wachina kumbe ni kwa sababu wanafanyakazi kwa uaminifu na hawagawani faida mpaka kazi iishe na kwao kuna sheria kali sana wakiharibu kazi huku ndiyo sababu wana nidhamu ya kazi kuliko sisi," alisema Waitara.

Anasema tamaa na ubinafsi umesababisha makandarasi wazalendo kushindwa kuungana ili wapate uwezo wa kimtaji na mitambo ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kama ilivyo kwa wenzao wa China ambao hawaweki ubinafsi mbele.

"Kuna watu wakiungana wakipata malipo ya awali tu wanapanda ndege kwenda Dar es Salaam kugawana fedha hata kabla ya mradi kuanza sasa mkifanya hivyo na mradi ukasimama fedha za kuendeleza mtazipata wapi," alihoji Naibu Waziri.

Aidha, Waitara alisema hata kama makandarasi wataungana na kutekeleza miradi mikubwa wanapaswa kugawana faida kidogo na kuacha mtaji wa kuanzia iwapo watapata kazi zingine kwani wengi wao hushindwa kuanza miradi mipya wanayoipata.

"Kuna mtu wanashangaza sana unakuta mtu hata kazi hajafika nusu ameshanunua gari la kifahari, kamnunulia mke wake gari la kisasa mambo ya kushangaza kabisa, kwanini usisubiri ukamilishe mradi wa watu uwe na amani ya kutumia fedha zako," alisema Waitara.

Pia aliwataka makandarasi hao kurejesha fedha wanazokopa kwenye benki mbalimbali ili wajenge uaminifu na wengine waweze kukopa na kinyume chake ni kusababisha benki hizo kushindwa kuwaamini wengine wanapokwenda kukopa.

Alisema CRB imeanzisha mfuko wa ambapo makandarasi wazalendo wa madaraja yote wanaweza kukopa lengo ikiwa ni kuwajengea uwezo hivyo ukuaji wake utategemea sana uaminifu wa marejesho ya fedha zitakazochukuliwa.

Alisema serikali itaendelea kutenga miradi ya kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo na amewataka kuonyesha uwezo kwa kukamilisha miradi watakayopewa kwa ubora wa hali ya juu na kwa wakati ili waendelee kuaminika kwa wateja.

Naibu Waziri pia alipongeza CRB kwa kuandaa mikutano ya mashauriano na makandarasi akisema kuwa inawapa mwanya makandarasi hao kubadilishana mawazo na ujuzi na wenzao na kueleza changamoto mbalimbali zinazowakabili ili zitatuliwe.

"Nawapongeza kwa kuandaa mikutano hii kwani hapa ndipo mnajipanga kuinua makandarasi, mnakosoana mlipokosea na mnashauriana namna ya kwenda mbele kwa hiyo sisi serikalini tunaiunga mkono mikutano hii iendelee kwa sababu faida zake ni nyingi kwa washiriki na nyinyi bodi," alisema Waitara.



Makandarasi wa ndani wana uwezo wa kujenga daraja kama hili kama wakiwezeshwa kiuchumi.

## SIKU KIMATAIFA DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA:

# Bangi imetumika zaidi kipindi hiki cha Covid-19

**Vienna,** AUSTRIA

IKIWA leo ni Siku ya Kimataifa dhidi ya Matumizi mabaya ya Dawa za Kulevya na Usafirishaji Haramu, ripoti mpya iliyotolewa na ofisi ya Umoja wa Mataifa inayohusika na dawa na uhalifu (UNODC), imeonya kwamba idadi ya watu wanaotumia mihadarati duniani, inaongezeka.

Shirika hilo katika ripoti iliyotoa jana, limesema kwamba mwaka jana, pekee, duniani kote takriban watu milioni 275 walitumia mihadarati, likiwa ni ongezeko la asilimia 22 tangu mwaka 2010.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa utafiti wa ofisi hiyo ambao pia unatoa mtazamo wa jumla wa soko la mihadarati duniani pamoja na athari zake kwa afya za watu na maisha yao katika mtazamo wa janga la corona au COVID-19.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya dawa za kulevya ya dunia ya UNODC-2021, matumizi ya bangi yameongezeka mara nne katika baadhi ya sehemu za dunia zaidi ya miongo miwili iliyopita, wakati asilimia ya vijana ambao walichukulia dawa za kulevya kama ni hatari ilishuka kwa asilimia 40.

Pengo la mtazamo bado lipo licha ya ushahidi kwamba matumizi ya bangi yanahusishwa na aina mbalimbali za athari za afya na madhara mengine, hasa kati ya watumiaji wa muda mrefu.

Aidha, nchi nyingi zimeelezea kuongezeka kwa matumizi ya bangi wakati wa janga la COVID-19. "Mtazamo wa chini wa hatari ya matumizi ya dawa za kulevya umehusishwa na viwango vya juu vya matumizi ya dawa hizo, na matokeo ya ripoti ya dawa za kulevya ya dunia ya UNODC ya 2021 inaonyesha haja ya kuziba pengo kati ya mtazamo na hali halisi kwa kuelimisha vijana na kulinda afya ya umma," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa UNODC Ghada Waly.

Uzinduzi wa Ripoti ya Dawa za Dunia ya 2021, umekuja katika kuelekea siku ya leo ya kimataifa dhidi ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya na usafirishaji haramu, ambayo huadhimishwa kila mwaka Juni 6. Kaulim mbiu ya mwaka huu ya kampeni inayoongozwa na UNODC ni "Sambaza ukweli juu ya mihadarati, okoa maisha" ili kufikia ulimwengu bila ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya.

**UN**



Wanaharakati wa mazingira wakisafisha takataka kwenye Mto San Juan, unaopita katika mji wa Mandaluyong nchini Philippines, juzi.
**PICHA: REUTERS**

# Museveni arejea maombi kitaifa kuikabili corona

**Kampala**, UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, alitenga siku ya jana kuwa ya mapumziko maalumu kwa ajili ya kuwaombea wahudumu wa afya pamoja na familia zilizoathiriwa na virusi vya corona.

Nchi hiyo ya Afrika Mashariki, inakabiliwa na wimbi la pili la virusi vya corona, jambo lililomsukuma rais kuweka amri ya kutotembea na kufungwa kwa shughuli' yaani 'lockdown" mapema mwezi huu. Bunge la Uganda, limefungwa kwa muda kwa wiki mbili huku maofisa wakisema watu 100 katika bunge, hilo walipatakana na maambukizi ya virusi hivyo.

Idadi ya vifo vilivyothibitishwa imeongezeka mara 10 katika kipindi cha siku 14 katika kulingana na wavutaji wa Our Word in Data, chini ya asilimia mbili ya watu ndio waliopokea walau dozi moja ya chanjo ya virusi vya corona.

Wakati hayo yakijiri, Uingereza imeipongeza Uganda katika orodha yake ya nchi ambazo raia wake wamezuiwa kusafiri kwenda nchini Ungereza.

Ofisi ya mambo ya kigeni na Jumuiya ya Madola (FCO), ilisema kuwa kuanzia Juni 30, mwaka huu, Uganda itahamia kwenye orodha nyekundu ya kuingia England.

**BBC**

# Watu 64 wauawa jeshi likishambulia soko

**Tigray,** ETHIOPIA

WATU 64 wameuawa na wengine 180 wamejeruhiwa baada ya ndege ya jeshi la Ethiopia, kushambulia soko katika Jimbo la Tigray Kaskazini mwa Ethiopia.

Mshauri wa kiongozi wa jimbo la Tigray Mulu Atsbaha, alisema shambulizi hilo lililenga soko katika mji wa Togoga na idadi ya watu waliopoteza maisha kwa mujibu wa maofisa wa afya, watu wengi wamejeruhiwa.

Jeshi la Ethiopia limekiri kutekeleza shambulizi hilo na kuongeza kuwa, lilikuwa likiwalenga wapiganaji wa jimbo la Tigray.

Hata hivyo, walioponea shambulizi hilo, walisema waliona mabomu kutoka angani yakiwalenga na kusababisha pia vifo vya watoto waliokuwa sokoni.

Umoja wa Mataifa (UN), umelaani shambulizi hilo na kutaka uchunguzi wa kina kufanyika na tukio hilo limetokea wakati wananchi wa taifa hilo wakisubiri matokeo ya uchaguzi wa wabunge uliofanyika siku ya Ju-

# Mauaji George Floyd, mwenye hatia kuadhibiwa miaka 30 jela

**Minneapolis,** MAREKANI

MAHAKAMA ya mji wa Minneapolis nchini Marekani, jana ilitaja adhabu atakayopewa Derek Chauvin, polisi mzungu aliyekutwa na hatia ya kumuua Mmarekani mweusi George Floyd.

Mwezi Aprili, mwaka huu, jopo la majaji maalumu lilimkuta Chauvin na hatia ya mauaji yasiyo ya kupanga, nchini Marekani yakijulikana kama mauaji ya daraja la pili.

Upande wa uendeshaji mashtaka unataka Chauvin apewe kifungo cha miaka 30 jela, huku upande wa utetezi ukitaka adhabu atakayopewa aitumikie bila ulazima wa kupelekwa gerezani.

Kifo cha kusikitisha cha Floyd kilichotokea Mei 25, mwaka jana, kilisababisha maandamano kote duniani, ya kupinga ubaguzi wa rangi na ukatilili wa polisi nchini Marekani.

Kifo hicho kilirekodiwa katika mkanda wa video, uliomwonyesha Ofisa Derek Chauvin akigandamiza goti shingoni mwa Floyd, akiwa amelala sakafuni kwa karibu dakika tisa, huku akilalamika kuwa hawezi kupumua.

Polisi walikuwa wamemkamata Floyd kwa tuhuma za kutumia noti bandia ya dola 20.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BETINA EDWARD MWAKYUSA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.219/12** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary SONGEA GIRL'S mwaka 1986,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/316254/2021**

116330102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO W A TANZANI**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MWANG'OMBE**

**Usimamizi wa mirathi Na. 34/2021**

**Ombi la SAFIA JUMA ULEDI kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu RUKIA MUSSA MAROWA**

**Kwa YOYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaomdai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 6/7/2021 Kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi w a mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani kukaguliwa. 24/04/2021

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANG'OMBE

116330802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI**

**LABOUR EXECUTION NA.17/2020**

**JERICO K.PWELE ..............................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

**OFF.ROUTE TECHNOLOGY (T) LTD......MLALAMIKIWA**

**YAH : WITO KWA:**
**MARY ELIZABETH**
**DAUDI NELBERT MBOMA**
**BRIAN MALCOM THOMSON**
**POPOTE MLIPO**

Mnatakiwa kufika binafsi mbele ya Mahakama hii itakayokaa Mbeya mnamo tarehe 02/07/2021,saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mhe. P.R.Kahyoza Msajiri, na kubakia mahakamani hadi Mruhusiwe na Mahakama kuondoka kwa ajili ya kusikilizwa kwa deni/tuzo
Na Mnataadharishwa kuwa msipuuze asilani kutii samansi hii,vinginevyo mtaadabishwa kwa kutozwa faini au kufungwa jela.
Imesainiwa hapa Mbeya siku ya Jumatatu,tarehe 14.mwezi Juni,mwaka 2021.

.......................................
**P.R KAHYOZA**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**

116330902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MJAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MWANG'OMBE**

**Usimamizi wa mirathi na.33/2021**

**Ombi la AHMED ATHUMANI MAKALO kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu MZEE ATHUMANI MAKALO.**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/7/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani kukaguliwa. Tarehe 24/06/2021

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANG'OMBE

116331002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILY KAVISHE**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA PASSO** yenye namba za usajili **T 617 DHG,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa
**DAR/URA/RB/317263/2021**

116330002

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**BAHATI WILSON** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S0549/0009** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary LUGOBA mwaka 2008, na cheti cha chuo cha (SLADS) SHOOL OF LIBRARY ARCHIVES AND DOCUMENTATION mwaka 2010 REGISTRATION NAMBA C/2009/1488,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa CONTROLO NAMBA **9910820275621**

116329202

---

**KATIK MAHAKAMA KUU TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 58 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SYLVESTER MOGA MACHILU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**ZIPORA SYLVESTER MACHILU**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahimishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5th mwezi july 2021.
Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 10th mwezi june 2021.

Imewasilishwa
NAIBU MSAJILI

116329302

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWANAIDI AWADHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S 0516-0503** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MOMBO mwaka 2015,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/316117/2021**

116329502

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi No.47/2021**

**Ombi la MARIA PAUL KUNAMBI kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu EMILIAN MSICHE CHAMLULU**

**KWA YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 3O/6/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 21/06/202

Tarehe 21/06/2021
Sahihi ya Hakimu

116329802

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.191/2021**

**Ombi la MAGRETH CHARLES TUMAI Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu VENANCIA VENANCY KAIZA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 19/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 17/06/2021

Tarehe 17/6/2021
Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116329902

---

NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street

P. O. Box 6707, Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045, Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

## MARUDIO YA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED,** tunatoa notisi ya siku tatu kulipa deni kwa hiari muda huo ukifika bila kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA,** Mnada utarudiwa siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, mnada utafanyika kuanzia saa 04:30 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.
**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA .**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | AVCC TRADERS | Hati Na. 100466, Kiwanja No.2016, Kitalu "B" Mbweni, Dar es Salaam City. Ukubwa wa eneo sqm 10959. | 29/06/2021 kuanzia saa 04:30 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki mnunuzi atakubaliana na benki
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi **piga simu No: 0782 065 914 / 0712 073 680**

116330302

---

## TANGAZO LA MNADA

**Umoja Professionals Limited (UPL)** na **AR Company LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba na viwanja katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam na Mwanza ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| SK Money 247 Company | Kiwanja kipo Kinondoni Mkwajuni-Dar | 13/07/2021 |
| Ramadhani Abdallahman Makuti | Kiwanja kipo Chamazi-Dar | 15/07/2021 |
| Emmanuel Simon Mwase | Nyumba ipo Temeke-Dar | 17/07/2021 |
| Jiloma Mayeka Kalemela | Nyumba ipo Kishiri -Mwanza | 15/07/2021 |
| Hezron Sigwa Barukuli | Nyumba ipo Nyasaka Godown-Mwanza | 16/07/2021 |
| Seveline Prosper katakweba | Nyumba ipo Buhongwa Mitimirefu-Mwanza | 19/07/2021 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0719336090(UPL-DAR) au 0768790047(FANIKIWA) au 0714680050(AR MWANZA**

1163309702

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**12**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

KWA upande wake Denny, pamoja na kuwa alikuwa Dar na kukutana na wanawake wengi, lakini alishangazwa na uzuri wa msichana huyo ambaye anaishi kijijini.

Si kwamba alitakiwa awe anaishi mjini kwa jinsi alivyo, lakini aliwazidi uzuri wasichana wengi mjini ambao wametumia gharama kubwa kwa kujipamba saluni na kuvaa nguo za gharama.

Alishangazwa na uzuri wa Bishara licha ya kwamba hakuwa anakwenda saluni, bila ya kuwa na nguo za gharama. Ni kama dhahabu iliyokuwa chini ya mchana au matope.

Aliona akiipeleka mjini itazidi kung'aa zaidi "Hivi huyu mtoto akifika mjini, aende saluni kuvaa nguo za gharama itakuwaje?" Alijiuliza.

Kingine ni ubichi wa msichana huyo. Alikuwa na miaka 23 tu. Alitokea kumpenda tangu siku ile aliupomwokoa kwa jamaa aliyetaka kumbaka. Lakini hakutaka kuchukua pupa wala haraka. Alijua muda utafika na kweli ulifika. Wote wawili walijikuta wako kwenye lengo moja.

Kila mmoja alimueleza mwezake kinachomsibu moyoni. Kila mmoja akimfungukia mwenzake.

Denny aliandika barua na kumwambia kwa sababu hatokuwa na mshenga, basi yeye mwenyewe Bishada ndiyo awe mshenga.

Bishada aliangua kicheko, akaichukua na kuipeleka kwa mama yake. Mama aliipokea kwa mikono miwili. Alijua kabisa kuwa hiyo itakuwa ni barua ya mwisho. Kwa sababu anayekataa kila barua inayoletwa hapo, ndiye aliyeleta barua hiyo.


Baada ya taratibu zote kufanyika, barua ile ikapelekwa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji.

Ilipelekwa kwa sababu maalum. Ni kwa sababu ilikuwa bado siku mbili tu ili wafurushwe kwenye kijiji hicho kama binti yao Bishada atakuwa hajaolewa au kuchumbiwa.

Angalau sasa mzee Ngoma na mkewe Fatuma walianza kuona mwanga. Nao ni wa kubaki kwenye kijiji hicho na pia binti yao sasa kupata mume.

**********************

Hali ilibadilika. Kijiji kizima kilijua kuwa Bishada amepata mchumba. Mchumba na Denis, kijana aliyetoka mjini kuja kijijini hapo kwa ajili ya kusimamisha urithi wa mashamba ya mjomba wake.




Mwenyekiti naye alikuwa ameshapelekewa nakala ya barua ya posa. Kwa hiyo zile siku mbili ambazo walitakiwa kuhama zilifutika.

Wale waliokuwa wakiionea familia hiyo kwa sababu ya kulipa kisasi waliufyata mkia. Si tu Bishada alipata mchumba, lakini alipata mlinzi pia.

Majaribio mawili ya kumdhuru msichana huyo yalizimwa kwa ustadi na Denny mwenyewe.

Vijana wa kijiji hicho waliishiwa pozi. Kuna wengine walidhani kuwa Denny bado anaishi kwenye nyumba ya mjomba wake.

Siku hiyo usiku wa manane moto mkubwa ulizuka kwenye nyumba hiyo. Watu waliamka na kukimbilia, lakini walikuta nyumba yote imeteketea.

Bishada alilia. Denny alimbebeleza. "Nyamaza mpenzi, hii si bahati mbaya. Ni makusudi."

"Kwa nini unasema makusudi?" Aliuliza huku machozi yakimtoka.

"Najua kuna watu walikuja usiku na kudhani mimi nimo ndani mle, wanachoma nyumba moto ili nifie ndani."

Bishada alishangaa.

"Ndiyo mpenzi. Ni kwamba bado kuna watu wanatutafuta. Wanataka kuniua mimi au wewe. Hapa kilichotakiwa ni kwamba mimi nife nikiwa ndani ya nyumba, ili nisikuoe."

Maneno hayo yalimfanya Bishada azidi kuangua kilio.

"Kumbe nimekuponza mpenzi wangu."

"Hapana. Hujaniponza. Walichounguza ni nyumba tu. Hawa hawakujua kuwa mimi siku hizi ninalala kwenu. Mimi ningeumia sana ungeumia wewe au mashamba ya mjomba wangu, lakini siyo nyumba. Nyumba ninayo. Ni ile ya baba yake mzee Ngoma."

Wiki moja ilipita baada ya tukio lile. Kijiji kilitembelewa na wageni. Alikuwa ni Mkuu mpya wa Wilaya. Alifika kutokana na malalamiko mengi kuhusu baadhi ya vijiji kutoendeshwa kwa haki.

Wenyeviti wa vijiji walikuwa kama miungu watu. Mkutano mkubwa ukafanywa. Malalamiko ya ubadhirifu wa fedha, rushwa na uonevu ulionekana kukithiri.

Mzee Mataulo, Mwenyekiti wa Kijiji hicho alikuwa mmoja wa viongozi waliotuhumiwa na rushwa, upendeleo na mengi yanayofanana na hayo. Akapigwa chini.

Kura ikamuangukia mzee Ngoma. Baba wa Bishada. Akaambiwa akaimu hadi hapo uchaguzi utakapofanyika baada ya miezi mitatu.

Wengi walianza kugeuka. Waliokuwa wanadhihaki na kumuonea mzee Ngoma kwa ajili ya binti yake, walianza kujipendekeza.

Mzee Ngoma hakuwa mtu wa visasi. Alitaka kijiji hicho kuwa kipya. Kuanza maisha mapya.

**Siku hiyo usiku wa manane moto mkubwa ulizuka kwenye nyumba hiyo. Watu waliamka na kukimbilia, lakini walikuta nyumba yote imeteketea.**

**********************

"Kesho tunaondoka." Denny alimwambia Bishada.

"Tunaenda wapi?"

"Mjini."

"Ndiyo."

"Kufanya nini?"

"Tunaenda kwangu ukakuone."

"Baba atakubali?"

"Nitamuomba."

"Atakubali?"

"Sijui. Ila nakuomba wewe ndiyo ukaombe. Najua hujakuwa mke, bado ni mchumba, lakini nimemaliza kila kitu hapa cha mjomba wangu. Nataka kwenda mjini kwanza, halafu baadaye nije kumaliza hili la harusi." alisema Denny.

Siku mbili baadaye Bishada alimwita Denny. Alipofika akambusu kwa furaha.

"Baba na mama wamekubali."

"Wamekubali?" Denny alishangaa.

"Ndiyo wanasema twende kwanza, halafu baadaye utanirudisha kwa ajili ya maandalizi ya harusi. Unajua Denny wazazi wangu wanakupenda sana. Ingekuwa mwingine hivi hivi tu, wala wasingekubali." Bishada alimpasha mpenzi wake.

"Najua. Hata wewe mwenyewe usingekubali kwenda." Alisema na kusababisha Bishada kuangua kicheko.

"Kwenda huko."

Wiki moja baadaye Denny na Bishada walikuwa wanaondoka kwenye kijiji hicho kwenda mjini.

Ilikuwa ni mara ya kwanza Bishada kuondoka kwenye kijiji chao alichozaliwa kwenda mjini.

Akili ilimrudisha mbali sana. Alivyokuwa akikataa wanamume kijiji hapo. Uhasama mkubwa uliozuka kiasi cha kuamuru kutimuliwa.

Alivyotakwa kubakwa na kuokolewa na mtu asiyemfahamu. Mgeni machoni mwake. Mtu huyo leo ndiye mchumba wake. Ndiye anayetarajia kumuoa. Hakufikiria kitu kama hicho maishani mwake.

"Mwanangu mjini huko. Kuwa makini. Umempata mchumba mwenye adabu zake. Huo ni kama mtihani. Umekataa wachumba wengi umemkubali wewe. Endelea na upendo wake kwake hivyo hivyo. Inawezekana kukataa wachumba kijiji, riziki yako ilikuwa mjini mwanagu," Mama alimwambia binti yake.

"Nimekuelewa mama yangu. Denny nimemkubali mwenye. Nampenda na sitomuacha."

"Twende."

"Nakupenda sana Bishada."

Nakupenda pia Denny."

**MWISHO**

# RASHFORD KUPASULIWA BAADA YA EURO 2020



**LONDON,** England

FOWADI wa Manchester United na England, Marcus Rashford atafanyiwa upasuaji baada ya michuano ya Euro 2020.

Rashford amekuwa akicheza na maumivu katika bega lake la kushoto aliloumia wakati wa mchezo dhidi ya Arsenal, Novemba mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amefunga mabao 21 na kutoa pasi za mwisho 15 kwenye mashindano yote kwa Mashetani Wekundu hao, atafanyiwa opereshini kuelekea kwenye msimu wa 2021-22.

Rashford mwenyewe amenukuliwa na BBC Sport akisema kwamba, huwenda akafanyiwa operesheni au asifanyiwe.

"Sina uhakika kwa asilimia 100 kama bado hahitaji kufanyiwa operesheni, hivyo nitakubaliana na lolote muda ukifika," alisema Rashford akinukuliwa na BBC Sport.

"Nitamaliza kwanza mashindano ya Ulaya na nitakuwa na wiki kadhaa za kusubiri na kuona nini cha kufanya."

Aliongeza: "Madaktari bado hawajasema. Sababu sijui ni lini itatokea hivyo, lakini kwa sasa nasubiri kwanza kujua."



# Benzema aweka wazi alichoteta na Ronaldo

**BUDAPEST,** Hungary

KARIM Benzema na Cristiano Ronaldo walionekana wakikumbatiana kwenye michuano ya Euro 2020 wakati Ufaransa ikicheza na Ureno Jumatano.

Mitandao ya kijamii iliibua hoja nyingi wakati wawili hao wakionekana kufurahia pamoja na kukumbatiana wakati wa mapumziko na baada ya mchezo huo kumalizika.

Wawili hao walihamia pamoja pale Santiago Bernabeu msimu wa 2009-10 na walifurahia mafanikio makubwa pamoja kabla ya Ronaldo - ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Madrid kuhamia Juventus.

Na sasa Benzema amenukuliwa akisema kile walichozungumza baada ya mchezo huo ambapo Ufaransa wa sare pale mjini Budapest na timu zote zikatinga hatua ya mtoano wa timu 16.

"Ni vizuri kumuona tena, tunatoka mbali," alisema Benzema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wote tumecheza miaka tisa au nane pale Real Madrid, na tulifunga mabao na kushinda mataji.

"Tulizungumza na tulitakiana heri kwa majaliwa yetu na klabu zetu na kwenye mashindano haya ya euro 2020."

Ronaldo amefunga mabao matano kwenye mashindano hayo na kufikia rekodi ya mabao 109 ya kimataifa iliyowekwa na Ali Daei wa Iran.

# Perez hajui hatima ya Varane Madrid

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez hana uhakika na majaliwa ya Raphael Varane hapo kwa miamba hao wa LaLiga akiwa anahusishwa na Manchester United, huku akikataa kuzungumzia kuhusu mpango wa kumwania Kylian Mbappe na Erling Haaland.

United imekuwa ikihusishwa na Varane na miamba hao wa Ligi Kuu ya England wakitajwa kwamba wanataka kumnunua nyota huyo wa Ufaransa kutoka pale Santiago Bernabeu kipindi hiki cha majira ya joto.

Chelsea na Manchester City pia zimeripotiwa kumwania mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu ya LaLiga tangu alipohamia hapo Madrid mwaka 2011.

Perez aliulizwa kuhusu majaliwa ya Varane na aliiambia El Transistor: "Sijui nini kitatokea kuhusu Varane.

"Yupo kwenye Euro na tutazungumza naye wakati atakaporejea.

"Tumepata ofa kumuhusu Varane. Kama atataka kuondoka atasema."

Madrid pia imekuwa ikihusishwa na nyota wa Paris Saint-Germain, Mbappe pamoja na straika wa Borussia Dortmund, Haaland.

Na kuhusu hao Perez amesema: "Mbappe? Sio mchezaji wa Real Madrid hivyo sikwezi kumzungumzia. Sijui nini mashabiki wanakitaka. Tupo kwenye harakati za kuijenga timu."



HABARI MICHEZO

# Daei ampongeza Ronaldo kwa rekodi

**TEHRAN,** Iran

MSHAMBULIAJI wa zamani wa timu ya Taifa ya Iran, Ali Daei amempongeza mshambuliaji na nahodha wa timu ya taifa ya Ureno, Cristiamo Ronaldo kufuatia nyota huyo kufikia rekodi ya mabao 109 katika michezo ya kimataifa.

Ronaldo alifikia rekodi hiyo baada ya kufunga mabao mawili kwa mikwaju ya penalti katika mchezo wao wa jana dhidi ya Ufaransa.

Daei aliwasilisha pongezi hizo kupitia mtandao wake wa kijamii wa Instagram ambapo ameandika: "Hongera sana Cristiano ambaye sasa umebakiza bao moja kuvunja rekodi ya kufunga mabao kwa wanaume kimataifa.

"Ni heshima kubwa kwamba mafanikio haya kwa sasa yatakuwa ya Ronaldo bingwa mkubwa wa soka na binadamu anayejali ambaye huchochea huwapa moyo wengine."






# MAN CITY YAKARIBIA KUMSAJILI GREALISH

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, kwa mujibu wa ESPN.

City ipo tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 100 kwa ajili ya kumsajili kiungo huyo, ambapo itakuwa rekodi kwa Uingereza kama watalipa kiasi hicho cha fedha na kuivunja ile ya Paul Pogba ya pauni milioni 89.3 ambayo Manchester United kumsajili mwaka 2016.

Grealish anajiandaa kuiwakilisha England kwenye michuano ya Ulaya hatua ya 16 bora dhidi ya Ujerumani na usajili wake kutua Man City ukitarajia kufanyika baada ya michuano ya Ulaya.

Fainali ya euro 2020 inatarajiwa kufanyika kwenye uwanja wa Wembley, Julai 11 mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ameichezea mechi 213 Aston Villa, akifunga mabao 32, tangu alipoanza kuichezea timu hiyo mwaka 2014.

Amecheza mechi tisa kwa kikosi cha England na alianza wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Jamhuri ya Czech, Jumanne.

# *White anukia kutua Arsenal*

**LONDON,** England

ARSENAL imefikia hatua nzuri katika mazungumzo na Brighton kwa ajili ya kumsajili mlinzi, Ben White.

Sky Sports imeripoti kwamba, ofa ya kwanza ya Arsenal ya pauni milioni 40 ambayo ilikataliwa na sasa inapanga kutoa pauni milioni 50.

Brighton haijaweza hadharani kiasi cha fedha inachokitaka kwa ajili ya kumuachia White huku mmiliki wa klabu hiyo, Tony Bloom amebainisha kuwa atakuwa tayari kumwachia kama atataka kuondoka.

Arsenal inaendelea na mazungumzo na White ikiwa inataka kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

White alikuwa na kiwango kizuri hapo, akiwa amecheza mechi 36 za Ligi Kuu baada ya kucheza kwa mkopo kule Leeds msimu wa 2019/20.

Aliisaidia Brighton kumaliza nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, huku timu hiyo ikiruhusu mabao 46 tu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE KUTUA MADRID BAADA YA EURO 2020

●●● Yapanga kutuma ofa nene, huku mwenyewe akiwa hana...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wanatumaini kumsajili fowadi wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe baada ya michuano ya Euro 2020, kwa mujibu wa gazeti la Marca la jana Ijumaa.

Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Real Madrid huku PSG wenyewe wakiwa wanapambana kuhakikisha wanambakisha nyota huyo wa timu ya taifa ya Ufaransa.

Mkataba wa Mbappe na PSG unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na bado hajaonesha nia ya kusaini mkataba na miamba hao wa jiji la Paris.

**Madrid ilijaribu kusamjili mara kadhaa msimu uliopita na wakati wa dirisha dogo la Januari alionekana kama angeelekea pale Santiago Barnabeu kabla ya dili hilo kushindikana.**

Na sasa kwa mujibu wa ripoti, Real Madrid wanajipanga kuhakikisha wanamsajili nyota huyo wakati wa dirisha la majira ya joto.

Taarifa zaidi zinasema kuwa, Mbappe mwenyewe ameonekana kuwa tayari kuondoka pale PSG kwa ajili ya kutafuta changamoto mpya.

Kwa mujibu wa Marca Madrid wanapanga kupeleka ofa yao kwa PSG baada ya michuano ya euro 2020 kwa ajili ya kumsajili Mbappe.

Hata hivyo, Mbappe pia alikuwa anahusishwa na Liverpool ambapo mwenyewe aliwahi kunukuliwa akisema ni shabiki mkubwa wa wekundu hao wa Anfield.

## ZISIKUPITE

### VILLA KUMBAKIZA GREALISH

ASTON Villa wanaamini wanambakiza kiungo wao wa kati, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, ambaye ananyatiwa na Manchester City, Chelsea na Manchester United. ***(Athletic, subscription required)***

### GREALISH ATAKIWA KUONDOKA

WAWAKILISHI wa Jack Grealish, wanapendekeza aondoke katika klabu ya Aston Villa, katika hatua ambayo itamwezesha kupata pauni milioni 100 akihamia Manchester City. ***(Sun)***

### ARSENAL WAMKARIBIA WHITE

ARSENAL wamepiga hatua kubwa katika mazungumzo yao na Brighton kuhusu mpango wao wa kumsajili Ben White mwenye umri wa miaka 23, ambao thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 50. ***(Sky Sports)***

### MCGINN KUUZWA

KLABU ya Brighton haina mpango wa kumuuza kiungo wa kati wa Scotland, John McGinn mwenye umri wa miaka 26, msimu huu wa joto, huku Liverpool ikitathmini uwezekano wa kumpata. ***(Express and Star)***

### MALEN KUPEWA MKATABA

LIVERPOOL imeanza mazungumzo na PSV Eindhoven kuhusu mkataba mpya na straika, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 22, ambaye anatarajiwa kugharimu karibu pauni milioni 34. ***(Sky Sport Germany, via Express)***

### BRAITHWAITE AWANIWA

KLABU za Brighton, Burnley, West Ham na Norwich City zinahusishwa na mshambuliaji wa Barcelona na Denmark, Martin Braithwaite mwenye umri wa miaka 30. ***(Sport)***

### SALIBA AGOMBEWA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 20, bado anapigiwa upatu kuondoka Arsenal kwa mkopo na klabu kadhaa za Ulaya zinamnyatia ikiwamo Nice aliyoichezea kwa mkopo msimu uliopita. Newcastle United, Southampton, na klabu za Ufaransa za Rennes, Marseille, Lille, na Bayer Leverkusen ya Ujerumani pia inamtaka. ***(Footmercato)***

### YAMTAKA MILENKOVIC

KLABU ya West Ham imewasilisha dau la pauni milioni 17 kumnunua mlinzi wa Fiorentina mwenye umri wa miaka 23, Nikola Milenkovic, lakini ofa hiyo iko chini ya kiwango cha fedha kinachotakiwa na klabu hiyo ya Serie A kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia. ***(Calciomercato)***

### PAVLENKA AWANIWA

KLABU ya Burnley inajiandaa kuwasilisha dau la kumnunua kipa wa kimataifa wa Werder Bremen na Jamhuri ya Czech, Jiri Pavlenka mwenye umri wa miaka 29. ***(Bild)***

HABARI MICHEZO

## Wachezaji Mwadui wanatafuta CV -Kocha

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Salhina Mjengwa, amesema kwa sasa wachezaji wake wanacheza kwa kujitengenezea vizuri 'CV' zao katika michezo iliyosalia kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo alisema kwa sasa hawana miujiza ya kuinasua timu hiyo kubakia kwenye ligi hiyo zaidi ya wachezaji wake kupambana kufanya vizuri katika mechi hizo ili kuweka 'CV' zao vizuri.

Alisema ana matarajio makubwa kuona wachezaji wake wanaendelea kuonyesha kiwango kizuri katika michezo iliyobakia ili kujiweka sokoni kwa kupata nafasi ya kushawishi timu za ligi kumchukuwa.

"Ni kweli tuko kwenye hali mbaya sana ya kushuka daraja, bado hatujakata tamaa tunahitaji kupambana katika michezo iliyobakia kwa ajili ya kutafuta heshima na nafasi katika timu zingine zitakazoshiriki Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Alisema nina matumaini mazuri ya kiwango cha wachezaji wangu kupata nafasi kwenye timu zingine kwa msimu ujao endapo timu hiyo itakaposhuka daraja.

## Mhariri Nipashe akosa mpinzani uchaguzi TWFA

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania, (TWFA) leo kinafanya uchaguzi wake mkoani Tanga, huku nafasi ya Katibu Mkuu inayogombewa na Mhariri wa michezo wa gazeti hili la Nipashe, Somoe Ng`itu ikiwa haina mpinzani.

Uchaguzi huo unafanyika kwa ajili ya kupata viongozi wapya baada ya wale walikuwapo madarakani muda wao kufikia mwisho.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Usajili wa TWFA, George Mushumba wagombea ambao wameingia kwenye uchanguzi huo, kwa nafasi ya mwenyekiti ni wawili ambao ni Amina Karuma anayetetea nafasi yake na Sara Chao, huku Makamu Mwenyekiti ikiwaniwa na Roseleen Kisiwa na Beatrice Mgaya.

Nafasi ya Katibu Mkuu inagombewa na mtu mmoja ambaye ni Somoe anayetetea nafasi yake na Katibu Msaidizi inawaniwa na Veronica William ambaye naye hana mpinzani.

Pia mjumbe wa mkutano mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Zena Chande naye amekosa mpinzani, kwenye nafasi za wajumbe ya utendaji wa TWFA.

"Mchakato umeenda vizuri na tumefanya usaili kwa uhakika juu ya wagombea ambao wanawania nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi na sasa wanatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa kama tulivyoanza salama hadi kufikia sasa," alisema Mushumba.

# RUVU SHOOTING, POLISI ZASIKITISHWA NA SARE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sare ya bao 1-1 juzi kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi, mkoani Pwani, makocha wa Ruvu Shooting na Polisi Tanzania wameeleza kutofurahishwa na sare waliyotoa kwenye mechi hiyo.

**Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, amesema kuwa mchezo ulikuwa mgumu sana na lengo lilikuwa na kupata pointi tatu ili kujiweka sehemu salama zaidi, lakini ikashindikana.**

"Mechi ilikuwa ngumu, kipindi cha kwanza tulitoka mapumziko tunaongoza. Kipindi cha pili tukafanya makosa wenzetu wakarudisha. Na tatizo nililoliona ni kwamba kipindi cha pili wenzetu walionekana kucheza vizuri zaidi kwa sababu tuliwapa nafasi kubwa ya kufikiri cha kufanya wakati wakiwa na mpira. Tulikuwa tunawaachia wanatuliza mpira, kufikiri na kujiandaa, badala ya kuwanyima nafasi hiyo," alisema Mkwasa.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema sare hiyo imemfanya kufikiria kushinda mechi zote mbili zilizobaki, kwani anachotaka ni kumaliza kwenye nafasi ya tano.

"Pamoja na kwamba tupo kwenye eneo salama, lakini tulitaka kushinda mechi hii ili tumalize kwenye nafasi ya tano kama ilivyokuwa msimu uliopita au juu ya hapo. Hilo ndilo lengo letu kuu msimu huu, kama tutamaliza chini ya hapo, hata kama hatukushuka, lakini tutakuwa hatukufikia lengo." Alisema Malale.

Kwa matokeo hayo, Polisi Tanzania ambayo ilikuwa ugenini, inashika nafasi ya saba ikiwa na pointi 42, huku wenyeji Ruvu Shooting wakiwa kwenye nafasi ya 10 kwa pointi 38, kila timu ikiwa imebakisha michezo miwili kumaliza ligi msimu huu wa 2020/21.




Rais wa RT, Silas Isangi (kulia), akikabidhi cheti kwa mwakilishi wa Silent Ocean Mohamed Kamilagwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Riadha yatoa cheti kwa wadau*

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKISHO la Riadha Tanzania (RT) limetoa cheti cha shukrani kwa wadau ambao wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali ikiwamo ya vyakula na fedha kwa ajili ya timu ya riadha iliyopo kambini Olimotonyi mkoani Arusha.

Timu hiyo itashiriki michezo ya Olimpiki nchini Japan kuanzia Julai 23 hadi Agosti 8, 2021, ambapo timu itaondoka Julai 29 hadi Nagai, Japan kupiga kambi kabla ya kwenda Tokyo kushiriki michezo hiyo.

Miongoni mwa wadau waliokabidhiwa cheti ni kampuni ya Silent Ocean, ambayo imesaidia timu hiyo vyakula vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 3 kwa ajili ya wanariadha waliopo kambini wakiendelea kujifua.

Akitoa cheti hicho jijini Dar es Salaam juzi, Rais wa RT, Silas Isangi, aliishukuru Silent Ocean na kusema imekuwa mstari wa mbele kusaidia mchezo wa riadha na hasa timu ya taifa inayojiandaa kwa Michezo ya Olimpiki ya Tokyo 2020.

"Tutahakikisha msaada unaotolewa na Silent Ocean kwa ajili ya timu iliyopo kambini, unatumika vizuri kwa malengo yaliyopangiwa ili kuleta maendeleo katika mchezo huo," alisema Isangi.

Naye mwakilishi wa Silent Ocean, Mohamed Kamilagwa, alisema, wameamua kuusaidia mchezo huo kwa kuwa watu wengi hawako mstari wa mbele kusaidia, licha ya kulileta sifa kubwa Tanzania kupitia kina Filbert Bayi, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na wengineo.

"Mchezo wa riadha umeliletea taifa letu sifa kubwa kuliko mchezo mwingine wowote kupitia kwa magwiji hao na wengineo, lakini hawapati udhamini unaostahili na ndio maana sisi tumeamua kuwasaidia," alisema Kamilagwa.

Alisema wataendelea kuusaidia mchezo huo na kama hali ya janga la virusi vya corona litatulia, basi wanatarajia kuipeleka China timu ya taifa ya riadha kwa ajili ya kambi ya muda mrefu.

Mratibu wa misaada hiyo, Nelson Mrashani, alisema, amekuwa akifanikisha kupatikana kwa misaada baada ya kuridhika na jitihada zinazofanywa na uongozi mpya wa RT wa kuuendeleza mchezo huo.

# Michezo

Jumamosi Juni 26, 2021

Nipashe




Mbappe kutua Madrid baada ya Euro UKURASA 22



Mchezaji wa Yanga, Tusila Kisinda (kulia), akiwatoka mabeki wa Biashara United wakati wa mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA baina ya timu hizo uliopigwa Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi mjini Tabora jana. Yanga ilishinda bao 1-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yatinga fainali

## ●●● Juhudi zake za kushambulia mfululizo zilizaa matunda dakika ya 22, baada ya Yacouba...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee la mchezaji raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne, liliifanya timu ya Yanga kutangulia kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, wakati ikiichapa Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mjini Tabora, jana.

**Ilikuwa ni mechi kali ya nusu fainali ya kombe hilo ambayo ilikuwa ikisubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi wa soka, ambao walifurika kwenye uwanja huo.**

Kwa ushindi huo, Yanga inamsubiri mshindi wa leo kati ya Simba dhidi ya Azam FC kucheza fainali kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma.

Hii ni mara ya kwanza kwa Yanga kutinga fainali hiyo tangu msimu wa 2015/16 ilipotinga hatua hiyo na hatimaye kutwaa Kombe la FA, ikiichapa Azam FC mabao 3-1

Dakika ya 12 tu ya mchezo, Deus Kaseke alikuwa karibu aipatie Yanga bao, alipoupiga kwa kisigino mpira wa krosi ya Tusisila Kisinda, lakini ukamgonga beki mmoja wa Biashara United, ukatoka nje na kuwa kona.

Juhudi za Yanga kushambulia mfululizo zilizaa matunda dakika ya 22, baada ya Yacouba kupachika bao kwa mguu wa kushoto, kufuatia mabeki wa Biashara United kukatika.

Bao hilo lilitengenezwa katikati ya uwanja kwa yeye mwenyewe Songne raia wa Bunrkina Faso, akammegea pande Feisal Salum, naye hakuwa mchoyo, akamtangulizia pasi moja safi na kumchambua kama karanga kipa wa Biashara United, Ssetuba James, mpira ukajaa wavuni.

Dakika za nyongeza za kipindi cha kwanza, kama mchezaji Deogratius Mafie angetulia, angeweza kuisawazishia Biashara United bao, baada ya kuukuka mpira ukizagaa kwenye eneo la hatari la Yanga, lakini alipiga shuti kali lililopaa juu ya lango.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, Yanga iliwatoa Yacouba aliyeumia na nafasi yake ikachukuliwa na waziri Junior, Kaseke akitoka na Saido Ntibazonkiza akiingia, huku Radhadhani Chombo 'Redondo' wa Biashara United akitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Kelvin Friday.

Ni kipindi ambacho kilitawaliwa zaidi na Biashara United ambao walijitahidi sana kushambulia, lakini tatizo lao lilikuwa ni umakini wanapofika kwenye eneo la mwisho.

Mafie, mchezaji pekee ambaye alionekana ni hatari zaidi kwa Yanga, aliachia shuti kwenye dakika ya 57, lakini lilichezwa kwa ustadi mkubwa na Farouk Shikalo, aliyeruka juu na kuugonga ngumi, mpira ikatoka na kuwa kona.

Mchezaji huyo huyo tena, nusura aisawazishie Biashara United dakika tisa kabla mechi kumalizika alipowatoka mabeki kadhaa wa Yanga na kuachia shuti la juu lililogonga mwamba, upande wa kushoto kwa kipa Shikalo, mpira ukarejea tena uwanjani.

# Simba, Azam ni vita vya Majimaji leo

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Kombe la FA Tanzania, Simba leo watakutana na mabingwa wa kombe hilo msimu wa 2018/19 Azam FC kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote mbili, kwani kila wanapopambana, mechi itakuwa kali, na ya kusisimua kwa mashabiki walio uwanjani na wanaofuatilia kwenye televisheni na redio.

Wakati Simba ikionekana kama kutaka kwenda fainali ikilitaka kombe hilo kwa ajili ya heshima na kulitetea, Azam inaonekana kulitaka kwa udi na uvumba kwani ndiyo safari ya uhakika zaidi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Kocha Mkuu wa Simba Didier Gomes amekiri kuwa watakuwa na kibarua kizito kucheza dhidi ya Azam FC kwani timu moja kati ya timu nzuri nchini.

"Utakuwa mchezo mgumu. Tunawaheshimu Azam kwa sababu tunajua uwezo wao, lakini sisi tumejipanga kufika fainali. Tunataka kushinda makombe yote, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho," alisema kocha huyo.

Alisema kwenye mchezo huo ni lazima wachezaji wake wacheze kwa kujituma na kuonyesha uwezo kama wanataka kufika fainali kwani malengo yao ni kushinda kombe hilo pia.

Nahodha wa timu hiyo, John Bocco ambaye anakwenda kukutana na waajiri wake wa zamani, alisema wanakwenda kukutana na timu nzuri na ngumu, lakini wao wamejipanga na Mungu atawasaidia.

"Tunakwenda kukutana na timu nzuri. Tunawaheshimu kwa hilo, lakini tumejipanga, Mungu atatusaidia kupata matokeo mazuri na kufuzu fainali." Alisema Bocco.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema mechi itakuwa ngumu kwa sababu ni timu moja tu inayotakiwa kuingia fainali.

"Tunaelewa umuhimu wa mechi. Tutapambana, haitokuwa kazi rahisi, lakini hatutowaangusha mashabiki wetu kwa sababu nia yetu kwenye kusaka nafasi ya kwenda fainali," alisema Bahati.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >